

# WILLIAMS AKUNWA KWA KIWANGO AFRIKA KUSINI

UKURASA 22

**SABAYA** aibukia kanisani, aomba radhi kwa wote aliowakosea

UKURASA 4



**SAMIA** atuma salamu kifo Rais Namibia

UKURASA 4

**KIWANDA** sukari Mkulazi chaanza uzalishaji, chatoa ajira kwa maelfu

UKURASA 8


# Nipashe

Jumatatu Februari 5, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581577

www.ippmedi...

...WANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com...

...an_newspaper


# Kinana atoboa tobo CHADEMA



**AANIKA** siri zao na CCM, adai chama hicho cha upinzani kimepewa na serikali bil. 2.7/-, wenyewe wacharuka... *Endelea ukurasa wa 2*

UKURASA WA 6

## WAAMUZI LIGI KUU CHEZESHENI KWA HAKI TUWAONE AFCON 2025

ILIPOTOKA orodha ya waamuzi watakaochezesha Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, inayoendelea nchin...




UKURASA WA 5

## LATRA YAKAMILISHA UKOKOTOAJI NAULI RELI YA SGR DAR-DODOMA

MAMLAKA ya Usafiri Ardhini (LATRA), imesema inakamilisha upangaji wa viwango vya nauli ya Reli...



UKURASA WA 20

## MALINDI YADUNDWA, YAIGEUKIA NGOME

TIMU ya Malindi SC imeanza vibaya Ligi Kuu ya Zanzibar mzunguko wa lala salama kwa kuambulia kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Wanajeshi wa Kipanga FC...

## Mtoto wa miaka 10 alea familia, Samia aahidi kumjengea nyumba ya kisasa

UKURASA 4

## Meli tatu zenye shehena ya sukari zapakuliwa bandarini

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA HESABU KWA DODOMA JIJI FC LEO UK. 24 **KATUNI** UK. 6

# Kinana atoboa tobo siri zao na CHADEMA

**Elizabeth Zaya na Maulid Mmbaga**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara amefichua sababu za kukwama kwa maridhiano kati yao na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) tangu Juni mwaka jana.

Abdulrahaman Kinana (pichani) ameweka wazi namna hoja 10 kati ya 12 walizokwenda nazo na kupata ufumbuzi ikiwamo serikali kuipa CHADEMA ruzuku ya Sh. bilioni 2.7 iliyoisusia kwa miaka mitatu.

Amesema CHADEMA ilipewa nafasi maalum ya kusikilizwa hoja zake. Matokeo ni pamoja na kesi 409 za wafuasi wa chama hicho zilifutwa na kubaki mbili zinazohusu mauaji mkoani Njombe na dawa za kulevya mkoani Pwani.

Akizungumza na wanachama wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam jana katika mkutano maalum, Kinana alitaja sababu za mkwamo huo zinazojumuisha CHADEMA kutumia lugha za udhalilishaji dhidi ya Rais Samia Suluhu Hassan kwenye mikutano ya hadhara na kulazimisha mchakato wa Katiba Mpya uanze ukihusisha vyama viwili (CCM na CHADEMA) ilhali ni jambo lenye kuhitaji kila Mtanzania. Ndani ya mchato huo, mna hoja nyingine ya kutaka serikali tatu.

"CCM tulipeleka hoja kwenye vikao vya mwisho tukiwaeleza kwamba tulikubaliana kutumia mikutano ya hadhara kujenga hoja, kunadi sera na tusitumie kukashifiana, kuzuliana na kukejeliana kiasi cha kusahau aliyeleta maridhiano ni Mwenyekiti wa CCM na Rais. Walitujibu 'jifunzeni kuwa na ngozi ya mamba'. Hayo si majibu ya kiungwana.

"Sasa mazungumzo hapo yalipofika yamekwama, tangu Juni hadi leo (jana) hatujakutana kwa sababu tuliwasihi mikutano ya hadhara isitumike kukashfu, kutukana na hasa kumdhalilisha kiongozi wa nchi, isemeni serikali na CCM lakini wanamtaja Rais kwa jina, tuliwaomba waache ila hawakuacha," alisema.

Kinana aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa CCM, alisema kuwa kuna wakati alikwenda kwa Rais na kumwambia kuwa mambo hayo ni magumu, lakini Rais Samia akamwambia aende nao polepole, akimtaja Mkuu wa Nchi huyo ni kiongozi asiye na papara, jeuri, wala hasira.

Alidai CHADEMA ilitaka suala la Katiba Mpya lizungumzwe kati ya vyama viwili bila kuhusisha wadau wengine, chama hicho cha upinzani kikishinikiza mazungumzo ya katiba yaanze kwao na vyama vingine vifuate baadaye huku wakitaka serikali tatu zitambuliwe kwenye Katiba.



Alisema katika kuandaa Katiba ya nchi lazima nafasi ya Rais ihusike, lakini CHADEMA walitaka kiongozi wa nchi asihusishwe katika suala hilo, akisisitiza katika taifa lolote duniani utaratibu huo haupo.

"Wakasema lazima kupunguza sana si tu nafasi ya Rais na ya serikali, wakatengeneza orodha ya watu ambao wanaweza kushiriki ikiwamo CCM na CHADEMA, wakasema kwenye vyama vingine chukua watu wawili au mmoja inatosha, viongozi wawili wa dini na nafasi za serikali hazina haja," alidai Kinana.

Kinana alisema CCM iliwaeleza CHADEMA kuwa Katiba haiwezi kuwa jambo la vyama viwili, taasisi zingine zikisikia jambo hilo haitakuwa sawa na kuwataka litafutiwe muda na namna nyingine ya kulitekeleza.

Alisema awali msimamao wa CCM ulikuwa kwamba wakati huu si mwafaka kwa Katiba Mpya, badala yake washughulike na masuala mengine kwa kuwa ziko nchi zina zaidi ya miaka 50 hazina Katiba, lakini CHADEMA wanataka kila baada ya miaka 10 ibadilishwe.

Alieleza kuwa hata sasa viko baadhi ya vyama vinataka mabadiliko madogo kwenye Katiba kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya uchaguzi wa 2024/25, akieleza kuwa mabadiliko hayo wanayataka kwa ajili yao.

"Sisi tuliwaambia kuna sheria zimepelekwa bungeni ya uchaguzi wa madiwani, wabunge na Rais, kuna Sheria ya Tume ya Uchaguzi na mabadiliko ya vyama vya siasa, lengo lake ni kuboresha mazingira ya uchaguzi 2024/25, tukasema si sawa itolewe bungeni na itolewe nafasi ya watu kushiriki.

"CHADEMA na wadau wengine walikuwa na maoni juu ya sheria hizi zilivyotolewa bungeni mwanzo, wakasema sheria mtakazopeleka bungeni zinazohusiana na Katiba, Tume ya Uchaguzi lazima ziende kwenye mchakato wa kawaida, CCM na serikali yake ikasema sawa zikafanywa taratibu zote mwezi wa 11, 2023 ikasomwa," alisema.

Kinana alisema CHADEMA hawakuamini kwamba Bunge lingetoa nafasi ya kutosha kwa wadau mbalimbali juu ya kutoa maoni yao kwenye Kamati ya Bunge la Katiba, Sheria na Utawala Bora. Lingesikiliza watu wachache na kumaliza, lakini jumla ya wadau 1,700 walisikilizwa na mjadala bungeni umechukua siku nne.

Kinana alisema mazungumzo yote na CHADEMA yalilenga kutatua hoja, malalamiko na matatizo ya CHADEMA ikiwamo viongozi wa CHADEMA waliokimbilia nje ya nchi. Ilifanyiwa kazi, wamerejea na hadi sasa wako salama na hawana kesi.

Pia alisema kulikuwa na hoja ya zuio la mikutano ya hadhara ambalo liliondolewa, lakini walijisahau na kuanza kumtukana, kumkejeli aliyeiruhusu badala ya kujenga hoja kwa wananchi.

"Hoja nyingine ni ya wabunge 19 hawajakaa kihalali bungeni. (CHADEMA) ni mabingwa wa kujenga hoja, walieleza mchakato mzima wa Kamati Kuu ya CHADEMA.

"Wakati tunazungumza, jambo hili lipo mahakamani. Kama kuna mahali Rais hana mamlaka nayo ni mahakamani, walitaka Rais asema zile kesi zote za mahakamani futeni, wale watoke na kuanzia leo siyo wabunge. Tuliwaambia hili hatuna mamlaka nalo, hili liko mahakamani na wanasheria wenu, nendeni mahakamani.

"Hoja nyingine, CCM imewaonea na kuwanyang'anya haki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019 na Uchaguzi Mkuu 2020, na walijibiwa uchaguzi umeshapita na lengo la kukaa ni yaliyojitokeza yasirudiwe lakini walitaka CCM itoe kauli kuwa yalifanyika madhambi mengi na kwamba walitengeneza kauli ambayo walitaka isomwe mbele ya umma, lakini walikubaliana kasoro zilizojitokeza zisijirudie na ndio maana zikaletwa sheria za uchaguzi ili kuwa na uchaguzi huru, haki na uwazi.

Kinana alisema duniani kote mazungumzo hayaishi mara moja. Kuna yaliyofanyika muongo hadi muongo na haiwezekani kufanya jambo likaisha mara moja.

**CHADEMA YAJIBU**

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia kauli hiyo ya Kinana, alisema sababu za kukwama kwa mazungumzo hayo ni CCM wenyewe kukataa hoja muhimu zilizowasilishwa na chama hicho.

"Nimemsikiliza Kinana na kwa sababu amezungumza muda mrefu, sisi kama chama tutakaa na tutatoa taarifa kuhusiana na hicho alichokizungumza, lakini leo (jana) ninatoa kauli ya awali. Kwanza ieleweke hajasema ukweli kuhusu sababu iliyosababisha mazungumzo kukwama," alisema Mnyika.

Katibu Mkuu huyo alisema kuwa miongoni mwa sababu za mkwamo wa mazungumzo hayo ni CCM kutokuwa tayari kuruhusu kurejesha mchakato wa Katiba Mpya ili kuwezesha Uchaguzi Mkuu ujao kuwa huru, kutokuwa tayari matokeo kupingwa mahakamani ikiwamo ya urais, kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi na mengineyo waliyopendekeza.

Mnyika pia alisema CCM haikuwa tayari kupeleka muswada bungeni kuendeleza mchakato huo wa Katiba kwa ajili ya kujenga mwafaka wa kitaifa.

"Na tulipeleka hadi ratiba ya namna mchakato wa marekebisho hayo ya Katiba unapaswa kufanyika ili kufanikisha kwa haraka kwa ajili ya kuwezesha uchaguzi wa 2025. Kwa hiyo, hayo mengine aliyoeleza Kinana hayana ukweli wowote," alisema Mnyika.

Awali Nipashe ilizungumza na Mkurugenzi wa Itikadi, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, ambaye alidai Kinana amepotosha.

"Kwanza kabisa, Kinana amefanya upotoshaji wa makusudi, ametafuta pa kutokea. Kwa mfano, kuna hoja ambazo amesema zilikuwa ni za kwetu binafsi wakati tuliwaambia kabisa kwamba hoja hizi zinatokana na kile walichokisema wananchi.

Mrema alisema CHADEMA haijawahi kufunga mlango wa mazungumzo hayo, bali ni CCM wenyewe wamekataa kusikiliza hoja za Watanzania.

Kuhusu ruzuku, Mrema alisema halikuwa jambo la hisani kwa sababu walistahili kupewa isipokuwa chama chao ndicho awali kilikataa kutoa akaunti ya benki.

Kuhusu wabunge wa viti maalumu, Mrema alisema jambo lililofanywa na chama hicho ni kuhoji sababu za wabunge hao kuendelea kuwapo bungeni wakati hawana chama wanachokiwakilisha.

"Anapozumgumza kwamba tulitaka wabunge waondolewe bungeni. Sisi tuliwauliza wanawakilisha chama gani wakati hawana chama na hata sheria inataka wabunge watokane na chama cha siasa? Wakati tunazungumza wakatuambia twende mahakamani, leo hii mahakama imeamua lakini bado wapo bungeni. Kwanini?" Mrema alihoji.

Kuhusu miswada mitatu iliyopitishwa bungeni, Mrema alisema kilichofanyika "ni kiini macho kwa sababu hakiko kwenye Katiba".

Tangu mwaka jana, CHADEMA, CCM na serikali walikuwa kwenye mazungumzo ya maridhiano kuhusu mambo mbalimbali yakiwamo yanayohusu mchakato wa Katiba mpya, maridhiano ya kisiasa na Tume Huru ya Uchaguzi.


**UBALOZI WA MAREKANI, DENMARK, UINGEREZA, WORLD BANK, CORUS INTERNATIONAL NA UMOJA HOUSE DAR ES SALAAM**

## MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Marekani, Denmark, Uingereza, World Bank, Corus International na Umoja house watauza kwa mnada wa hadhara Fanicha, Magari na Generator tarehe 10 February, 2024 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

Fanicha zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi: Sofa set, Sofa bed, Chest drawer, Meza za chakula/Viti, Book case, Dresser, Recliner, Meza za ofisi/Viti, Meza za mkutano/Viti, Steel cabinets, Vitanda, Magodoro, Fridge double door, UP Right freezer, Washer, Dryer m/c, Majiko umeme/Gas, A/c split unit, Mashine ya kukausha matunda kwa jua, (Solar Dryer), safe, Simtank 1000, 3000 Lts, Sports Baiskeli, na vingine vingi.

**Magari na Genereta yataanza kuuzwa Saa 6:00 mchana**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Toyota L/ Cruiser Prado TX S/ Wagon | 1KD Diesel Engine | 2016 | Haujalipwa |
| 1 | Toyota L/ Cruiser V8 Station Wagon | IVDO Diesel Engine | 2009 | Umelipwa |
| 1 | Nissan Patrol Station Wagon | TD42 Diesel Engine | 2009 | Haujalipwa |
| 1 | Suzuki Grand Vitara Station Wagon | J20 Petrol Engine | 2006 | Umelipwa |
| 1 | Ford Everest Station Wagon | WLAT Diesel Engine | 2004 | Umelipwa |
| 2 | Generators 500 KVA 3 Phase 415V | Perkins Diesel Engine | 2001 | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 7 mpaka 9 February 2024, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**AUCTION CONDITIONS:**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari au Generator atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 16 February, 2024 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Genereta litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya **VISA na Master cards za CRDB na NBC** yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu atatakiwa lazima kuwa na bid namba itakayopatikana getini na kuvaa barakoa.

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE DAR ES SALAAM**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926** **E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

## HABARI KITAIFA

# TPA yapokea shehena meli tatu sukari

## -ACT-Wazalendo yahadharisha ukali wa maisha

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI Chama cha ACT- Wazalendo kikiitaka serikali kuchukua hatua kutatua tatizo la sukari nchini kutokana na kuongeza ukali wa maisha ya watu wenye kipato cha chini, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), imesema imepokea meli tatu za bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi zilizoagizwa na Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), kupunguza uhaba.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Waziri Kivuli wa Viwanda na Biashara wa ACT- Wazalendo, Halima Nabalang'anya, alisema kupaa kwa bidhaa hizo ni maumivu makubwa kwa wananchi.

Alisema sukari imepanda bei maradufu kutoka Sh. 2,500 mpaka 2,800 Juni, mwaka jana hadi Sh. 4,800, 5,500 na 6,000 huku baadhi ya maeneo ikiwa haipatikana na kusababisha gharama za maisha kupaa.

"ACT tunaona kabisa hatua na miongozo ya serikali, haisaidii hata kidogo kutoa nafuu ya bei ya sukari tofauti na ahadi na hadaa inazozitoa. Kushindwa kuzalisha mahitaji yetu ya ndani ni sababu kubwa sana inayofanya tushindwe kudhibiti upandaji wa bei za bidhaa mara kwa mara.

"Uwezo wetu wa kuzalisha bidhaa kwa matumizi yetu ya ndani ni mdogo sana. Mfano mahitaji ya sukari kwa mwaka ni tani 585,000 wakati uwezo wetu wa kuzalisha sukari ni tani 370, 000 kiasi kinachopelea ni tani 215,000 tunaagiza kutoka nje," alisema Halima.

Alisema serikali imekuwa na wepesi wa kutoa vibali vya uagizaji wa sukari kuliko utoaji wa vibali vya uzalishaji na kuhakikisha kunakuwa na viwanda vyakutosha kuzalisha bidhaa hiyo nchini na kwamba kila mwaka uhaba hujitokeza.

"Tatizo la sukari kibiashara ni kama lango la ulanguzi na kujilimbikizia mali kwa baadhi ya wafanyabiashara waagizaji. Hivyo, uzalishaji wa sukari ndani kwao unawaondolea faida ya ziada (surplus profit) ndio maana zipo hisia au ushahidi wa kukamatwa kwa zaidi ya tani 40 mkoani Mtwara iliyofichwa kama njia ya kutengeneza uhaba ili kupandisha bei," alifafanua.

Alihadharisha kuwa waumini wa dini ya Kiislamu wanakaribia mfungo wa Ramadhani na wa dini ya Kikristu wanaingia katika Kwaresma katikati ya mwezi Februari, ni lazima serikali iondoe adha hiyo ili wananchi wasipate shida.

"Tunaitaka serikali iweke nguvu kubwa kuhakikikisha upatikanaji wa kutosha nchini, serikali kupitia vyombo vyake ifuatilie mwenendo wa uingizaji, uuzaji na usambazaji wa sukari ili kuhakikisha bei inashuka na wananchi wanapata sukari kwa wakati na kwa bei nzuri.

"Pili, tunaitaka serikali kuongeza kasi ya uwekezaji na uzalishaji katika viwanda kwa kuweka mazingira bora ya kisera na kisheria na kuchochea matumizi ya teknolojia za kisasa iongeze nguvu kwa kiwanda chake cha sukari cha Mbigiri (MKULAZI) ambacho kwa sasa kinazalisha tani 46 tu za sukari kiwe na uwezo mkubwa wa kuzalisha sukari ili kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali katika soko," alishauri.

Wakati ACT ikitoa hadhari hiyo, Mkurugenzi wa TPA, Bandari ya Dar es Salaam, Mrisho Mrisho, alithibitisha kupakua meli tatu zenye kontena za sukari wakati akizungumza na waandishi wa habari jana.

Alisema meli moja inabeba kontena 3,000 kwa meli tatu ni sawa na kontena 9,000 za bidhaa hiyo zilizoingia nchini kupitia bandari hiyo.

"Bandari ya Dar es Salaam tulipokea taarifa kutoka Bodi ya Sukari kuwa kuna meli tatu zenye bidhaa ya sukari ambazo tunatakiwa kuzifanyia kazi zitoke mapema. Ni kweli Januari 29 iliwasili meli ya kwanza na ilipokewa na kupakuliwa mzigo wote siku hiyo hiyo, lakini meli nyingine mbili zilichelewa," alisema Mrisho.

Alisema kuwa meli nyingine mbili ziliwasili Februari 2, mwaka huu na kufanyiwa kazi kwa wakati na mizigo yote kushushwa kama ilivyotakiwa kwa maslahi ya taifa. Alisema meli hizo zilipishana kutokana na foleni ya nchi jirani ambako zilikuwa zikishusha mizigo mingine kabla ya kuja nchini na sio kweli kuwa mzigo ulichelewa bandarini hapo.

Januari 20, mwaka huu, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema serikali imechukua hatua kadhaa za kumaliza uhaba wa sukari nchini ikiwamo kutoa vibali vya kuruhusu uingizaji wa sukari wa takriban tani laki moja kutoka nje.

Hatua hiyo imetokana na kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo kuuzwa Sh. 2,700 -3,000 hadi Sh. 4,000 -5,000 na katika baadhi ya maeneo kutopatikana kutokana na sababu zilizotajwa kuwa viwanda vinavyozalisha nchini kushindwa kufanya kazi kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha nchini.

Nchini kuna viwanda saba vya sukari, vikubwa kati ya hivyo ni Kilombero, ambacho kwa siku kinazalisha tani 700 za sukari, hata hivyo kiwango kimeshuka hadi 250, TPC kwa siku tani 450, lakini kwa sasa kimesimamisha uzalishaji kutoka na hitilafu za mashine, huku Kagera Sugar kikiwa na uwezo wa kuzalisha tani 500 kwa siku na sasa kinazalisha wastani wa tani 200 hadi 300.

Viwanda vyengine ni Mtibwa na Bagamoyo na kwa mujibu wa serikali, kutokana na mvua kubwa zinazoendelea, uzalishaji umepungua kwa takribani tani elfu moja kwa siku.

Pia inadaiwa kuwa mvua imeathiri hali ya uvunaji wa miwa mashambani kwenda viwandani na kupunguza kiwango cha sukari katika miwa kwa zaidi ya asilimia 25.

Siku za karibuni serikali imewakamata na kuwafikisha kwenye vyombo vya dola wafanyabiashara wanaoficha au kupandisha bei ya bidhaa hiyo.

***Imeandikwa na Mary Geofrey, Halfani Chusi**

# Operesheni ondoa mabango yasiyo na maadili yaanza

**Na Jenifer Gilla**

MKUU wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, jana ameongoza operesheni ya kuondoa mabango yaliyowekwa kinyume cha utaratibu kwa kutosajiliwa wala kulipiwa kodi katika wilaya hiyo huku mengine yakihamasisha uvunjifu wa maadili.

Akizungumza na waandishi wa habari, alisema wamegundua kuna mabango mengi yamebandikwa bila kufuata utaratibu wa kupewa kibali, kulipiwa kodi na mengine yamesajiliwa, lakini bado yanadaiwa hali inayoitia hasara halmashauri hiyo.

Alisema baadhi ya mabango hayo yanatangaza mambo yasiyoendana na maadili ya kitanzania na mengine kusababisha migogoro katika jamii ikiwamo watu kudhulumiwa.

Baadhi ya mabango hayo alisema yanadhalilisha wanawake kwa kuwataka walipie hela ili wawatafutie wanamume wa kuwaoa, mengine yenye viashiria vya utapeli wa ardhi kinyume na maadili na utamaduni wa Watanzania.

Kadhalika, ni chanzo cha uchafuzi wa mazingira kwa kubandikwa kwenye maeneo yasiyo rasmi ikiwamo kwenye nguzo za umeme na kuta zinazoangalia barabarani na kuwataka wahusika kuacha tabia hiyo, atakayebainika adhabu kali itachukuliwa dhidi yake.

"Tumeamua kuendelea na operesheni ya kuyaondoa mabango yote ambayo yanabeba ujumbe usiokuwa rafiki kwa maendeleo yetu ikiwamo wizi na utapeli, hayajasajiliwa na hayalipi ushuru katika manispaa yetu," alisema Mtambule.

Aliwasisitiza wafanyabiashara kufuata utaratibu wa kisheria kwa kuyasajili na kuyaweka maeneo waliyopangiwa, ili kuwapo na uratibu mzuri usioleta usumbufu kwa watu na mazingira.

Mhasibu wa Manispaa hiyo, Haruna Moshi, aliwakumbusha wafanyabiashara walioweka mabango yao katika wilaya hiyo na hawajalipia wafanye hivyo kabla hayajabomolewa.

Alisema kwa sasa wameanza kubomoa mabango yaliyowekwa bila kufuata utaratibu na baada ya wiki mbili watahamia kwa yasiyolipiwa kama wamiliki wasipotimiza wajibu wao.

Alisema kutokulipwa kwa kodi hizo kutasababisha halmashauri kutotimiza malengo ya kukusanya kodi ya Sh. bilioni 2.5 kwa mwaka huu wa fedha kwa kuwa mpaka sasa wamekusanya Sh. milioni 815 pekee.

Mwekahazina wa manispaa hiyo, Onesmo Mwonga, aliwakumbusha wafanyabiashara wanaotaka kuweka matangazo katika wilaya hiyo kufuata utaratibu, ikiwamo kuomba kibali na kulipa ushuru.

Alisema operesheni hiyo ni endelevu na watakaoondolewa mabango yao watalazimika kwenda kulipia gharama za kuyaondoa.


ZEUS RESOURCES

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST (EOI)-DIAMOND AND AIRCORE DRILLING**

**Title of the EOI:** Surface Exploration diamond drilling at its Mkuju Uranium Project

**Date of this EOI:** 5th February 2024

**Closing Date for Receipt of EOI:** 19th February 2024

**Address EOI Response by E-mail to the Attention of:** Technical Director

**E-mail Address:** zeustanzania9@gmail.com

**DESCRIPTION OF REQUIREMENTS**

1. Zeus Resources Tanzania Limited a subsidiary of Gladiator Resources Limited is issuing this Request for Expression of Interest (REOI) to seek interest from qualified Local and International Companies/Contractors with expertise and relevant experience, domestically situated for pre-qualification as a potential service provider. The planned program is an initial 2000m diamond core drilling a spart of early-stage exploration. Holes will be a maximum of 220 m in depth and will be vertical, drilled in NQ. The host rocks are Karoo Supergroup. The Project located in approximately 50 km east of Namtumbo in the Ruvuma Region Southern of Tanzania. Scope of the drilling program may expand for additional metreage depending on results of the initial drilling. Interested drilling contractors must demonstrate their capability in terms of equipment and experiences for this type of drilling, formation and conditions. Holes will be logged through casing using downhole geophysical tools. Contractors should describe their experience and suitability of equipment for the conditions and requirements stated above.
2. Contractors expressing interest should note that this REOI serves as a pre-qualification of the Companies that will be invited to participate in the Bidding process that will follow. As explained in the detailed REOI (to be provided) Mandatory Requirements, only contractors that meet the minimum pre-qualification criteria set out in this REOI will be invited to participate in the ensuing competitive bidding exercise.
3. This call for EOI does not constitute solicitation. Zeus Resources Tanzania Limited reserves the right to change or cancel the requirement at any time during the EOI.
4. Applicants may ensure better understanding of the opportunity and the requirement of the Expression of Interest by contacting Ryoba Chacha at zeustanzania9@gmail.com

**PRE-QUALIFICATION SELECTION PROCESS AND EVALUATION CRITERIA**

(a) Interested Vendors/Contractors will be pre-qualified through the pre-qualification evaluation criteria stipulated in the detailed REOI.

(b) Applicants/interested parties can obtain the project scope in the detailed REOI by emailing zeustanzania9@gmail.com. A hardcopy will also be available at **Zeus Resources Tanzania Limited,** located along **Yacht Club Road, House 19. Dar es Salaam Tanzania.**

(c) While preparing and sending their responses to this REOI, Contractors are requested to take note of important REOI dates as outlined below. Contractors will be notified in case of any changes in the dates indicated below:

(i) REOI Publication date: 5th February 2024
(ii) Deadline for posing REOI related questions and clarifications: 14th February 2024 at 16:00hrs Tanzania local time;
(iii) Deadline for responding to REOI questions and clarifications 16th February 2024 at 16:00 hrs. Tanzania Local Time;
(iv) REOI Closing Date: 19th February 2024 at 16:00 hrs, Tanzania Local time.

**NOTE**
**Information of the Company's Projects is available free of charge at the following address Projects – Gladiator (gladiatorresources.net)**



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda (mwenye kipaza sauti), akizungumza katika mkutano kati yake na madereva wa bajaji wa kituo kikuu cha mjini Musoma juzi, alipokwenda kusikiliza kero zinazowakabili ili kuzitafutia ufumbuzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtoto wa miaka 10 alea familia, Rais Samia kumjengea nyumba

**Na Beatrice Shayo,** KIGOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameahidi kumsomesha Alhaji Abdallah (10) na wadogo zake watano baada ya mtoto huyo kuacha shule akiwa darasa la tatu kutokana na ugumu wa maisha na kulazimika kuuza ndizi ili kuisaidia familia yake ya watu sita.

Pia ameahidi kuwapatia kiwanja na kumjengea nyumba mama yao, Ester Hussein ambaye ni mgonjwa na ujenzi utaanza Februari 9, mwaka huu.

Juzi Alhaji aliomba kipaza sauti katika mkutano wa Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, ili kuwasilisha kero yake, akiomba awezeshwe kupata elimu kwa kuwa mama yake hana uwezo wa kumsomesha na yeye anafanya biashara hiyo ili wapate chakula.

Alisema mama yake alikuwa anasumbuliwa na maradhi ya kuvimba tumbo, hivyo inamlazimu kuzunguka mtaani kuuza ndizi ili wapate fedha ya kununua chakula na kulipa kodi ya chumba kimoja wanamoishi ambacho gharama yake ni Sh. 20,000.

Makonda baaada ya kumsikiliza mtoto huyo alimwahidi kuwa CCM itamsomesha na kuwaomba viongozi kulisimamia jambo hilo ili ikiwezekana aanze shule Jumatatu (leo) na kumchangishia fedha ambazo zilipatikana Sh. milioni 2.22.

Jana Makonda alikwenda kuitembelea familia hiyo na kumpatia ujumbe wa Rais Samia kuwa ataisaidia familia hiyo ikiwamo kuwasomesha watoto wote watano na kulipia vifaa vyote vya shule na sare.

"Rais Samiaameguswa na maisha ya Alhaji, ameona upendo aliona namna alivyokuwa anapigania maisha ya mama yake na wadogo zake na kipaji chake ya biashara kwa sababu alikuwa anatunza fedha kutoka Sh. 4,000 hadi kufikia Sh. 20,000.

"Kwa kuwa yeye ni mama, anajua mateso, changamoto ambazo wanapitia kinamama, ameamua kukubariki kupitia Alhaji. Alhaji Rais Samia amenituma nikuambie anakujengea nyumba na ndani ya mwaka huu itakuwa imekamilika na tayari mtendaji wetu wa serikali wa mkoa wanatafuta kiwanja na fedha imeshatolewa ya kujengwa nyumba mpaka ikamilike na kuwekwa vifaa kama viti, meza na vitanda," alisema.

Makonda alisema jambo la pili aliloagizwa na Rais Samia ni kuhakikisha mtoto Alhaji anapata haki ya elimu na kumpatia mama yake mtaji wa Sh. milioni tano.

Makonda alisema Rais Samia pia atagharamia matibabu ya huduma ya afya kwa mama Alhaji na tayari Mkuu wa Mkoa wa Kigoma ameelekezwa kuhakikisha mama huyo anafikishwa hospitalini na kufanyiwa uchunguzi wa tatizo alilonalo.

"Hizo ni salamu za Rais Samia, kuwapata watoto wa aina hii katika kipindi hiki kuhangaika kwa ajili ya familia si jambo rahisi na hata katika ule mkutano alikuja kwa ajili ya kufanya biashara," alisema.

Ester alishukuru kwa msaada aliopatiwa na Rais Samia na kumwomba aendelee kuwa na moyo huo wa kuwajali wajane na yatima huku akihamia kwenye kilio kwa dakika kadhaa kutokana na ushujaa wa mwanawe.

**RAMBIRAMBI**

Katika hatua nyingine, Rais Samia ameungana na viongozi wenzake barani Afrika kutuma salamu za rambirambi Namibia kufuatia kifo cha Rais wake, Dk. Hage Gottfried Geingob kilichotokea jana.

Rais huyo alifariki dunia katika Hospitali ya Lady Pohamba iliyoko Mji Mkuu wa Windhoek, alikokuwa anapatiwa matibabu ya maradhi ya saratani.

Mkurugenzi wa Mawasiliano Ikulu, Zuhura Yunus, alisema Rais Samia amesikitishwa na kifo cha kiongozi huyo ambaye alikuwa rafiki wa muda mrefu na mwanajumuiya wa Afrika. Taarifa hiyo ilieleza kuwa Rais Samia ametuma salamu za rambirambi kwa wananchi, serikali, mke wa marehemu, Monica Geingob, ndugu, jamaa na marafiki.

# TCRA yashirikisha wadau kuleta ufanisi, huduma utangazaji, posta

**Na Mwandishi wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema inashirikiana na wadau mbalimbali kuboresha maudhui ya utangazaji ili kulinda tunu za taifa na kupanua wigo wa utoaji huduma za posta nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo kwa watoa huduma za posta, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisema lengo la ushirikishwaji huo ni kuhimiza uandaaji wa maudhui inayozingatia maadili ya kitanzania na kanuni.

Alisema utangazaji ni njia pekee ya mawasiliano inayowafikia watu wengi kwa haraka na wakati mmoja na kuongeza kwamba TCRA ina wajibu wa kuweka mazingira rafiki ya kusambaza huduma za utangazaji kwa njia ya redio, televisheni na mitandao nchi nzima ili kumfikia kila mwananchi.

Dk. Bakari aliainisha hatua zinazochukuliwa na TCRA kuhakikisha kuwa maudhui yanayorushwa na vituo vya utangazaji yanazingatia maadili na weledi wa uandishi wa habari na pia hayakiuki sheria na kanuni.

Alisema TCRA inahimiza utengenezaji, uzalishaji na usambazaji maudhui ya ndani na kutangaza urithi, vivutio, mila na desturi za Mtanzania.

"TCRA imeandaa vipindi maalumu vya redio vitakavyotoa elimu kuhusu uzingatiaji wa maadili, mila, desturi na utamaduni wa Mtanzania. Vipindi hivyo vilizinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Desemba mwaka jana. Kwa kuanzia vitarushwa na vituo 150 vyenye leseni ya kiwilaya ya utangazaji wa redio," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, TCRA inashirikiana na waandaaji binafsi wa maudhui ya ndani ili yawe na ubora na mipango imekamilika kuwezesha utoaji mikopo kwa masharti nafuu kwa watengenezaji maudhui binafsi na vituo vya utangazaji ili kukabiliana na changamoto ya raslimali fedha kwa watu wenye vipaji vya kuandaa maudhui bora ya ndani.

Aidha, alisema TCRA kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), imeendelea kuratibu kazi ya kurekodi ngoma za asili za makabila 120 kwa ubora wa hali ya juu ili kukuza utamaduni wa Tanzania.

"Mpaka sasa makabila 10 ya Kitanzania yamerekodiwa. Wataalamu wa masuala ya historia za makabila wataandika makala yanayohusu kila kabila, ili kuwa na kumbukumbu ya vizazi vyote. Zoezi hili litafanyika kwa awamu nne," alibainisha Dk. Bakari.

# Sabaya aibukia kanisani, aomba radhi aliowakosea

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amejitokeza hadharani kwa mara ya kwanza tangu alipoachiwa huru baada ya kushinda kesi zake, akiomba msamaha kama kuna Mtanzania aliyemkosea huku akisema kwa sasa hatapigana vita na mtu yeyote.

Pia amesema kuwa kwa watu ambao waliomkosea, amewasamehe, hivyo ni wakati wa kuanza upya kwa watu kuishi kwa amani na upendo badala ya kuendeleza chuki.

Ole Sabaya aliyasema hayo jana jijini Arusha akiwa kwenye ibada ya shukrani katika Kanisa la Ebenezer Restoration Ministry lililoko Suye, Kata ya Kimandolu.

Alisema kama kuna mtu yeyote atakayeendeleza vita, ataiacha vita hiyo mbele ya kanisa kwa kuwa yeye na amenyanyua mikono juu, hatopigana vita, kugombana na mtu, amesamehe kila mtu.

"Ninatangaza kwenye madhabau japokuwa maneno mengi yalizungumzwa na watu wengi wakadhani pengine nimewakosea, pia wako ambao siwafahamu wakanunua yale maneno wakidai Sabaya ni mbaya.

"Wakatengeneza cheni kubwa kwa kadri wanavyoweza na nimesimama kwenye madhabau hii kwa kuwa ninataka kusema kama kuna mtu nimemkosea, na kwa moyo wake wote anajua nimekosea yeye mbele za Mungu, ninaomba anisamehe.

"Na mimi ninasema mbele ya Mungu kama kuna mtu yeyote anadhani alinikosea iwe shahidi au kwa kutengeneza kesi kwa kunisingizia na kunisemea uongo popote, nimesema (leo) jana kwa kibali cha Mungu nimemsamehe na ijulikane kuwa Mungu wa madhabau hii amenipatanisha mimi na watesi wangu," alisema Ole Sabaya.

Alisema anamshukuru Mungu, watu waliomwombea, majaji waliotenda haki na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa wamefanikisha mpango wa kuboresha mifumo ya mahakama ya utoaji haki kwa wananchi.

Vilevile, alisema kuwa alipokwenda gerezani kwa mara ya kwanza Aprili 4, 2021, alikuta kuna mrundikano wa watu mahabusu lakini wakati akiondoka huko, kutokana na mfumo rafiki uliowekwa na serikali, watu ambao kesi zao hazikuwa zinaeleweka waliachiliwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa na walibaki watu 180.

Alisema kuwa akiwa jela baada ya kufungwa miaka 30, watu wasiopungua 248 kwa siku moja walikwenda kumtembelea kwa kuwa walionesha upendo wa hali ya juu kwake.

Askofu wa Kanisa la Kilutheri Afrika Mashariki (KKAM), Dk. Philemon Mollel, alisema watu walifika katika kanisa hilo kwa ajili ya kumshukuru Mungu kwa alichomtendea Sabaya wala siyo kumsafisha.

Mama mzazi wa Ole Sabaya, alisema kutokana na mapito magumu aliyopitia kijana wake, walikaribia kukata tamaa lakini Mungu alimtia nguvu.

Naye Jesca Nassari, mke wa Sabaya, alisema kuwa siku ya jana ni ya kipekee kwao na yenye hisia kutokana na matatizo yaliyowakumba.

"Ukiwa na neema ya Mungu haupungukiwi na kitu chochote. Kama ilivyokuwa kwetu tulikuwa na imani kwa kuwa wamtumainio Mungu ni kama Mlima Sayuni, hawatatikisika milele," alisema Jesca.

# Kahyarara: Tumieni Bandari ya Kwala kuondoa foleni Dar

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara, ameipongeza Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), kwa kuimarisha Bandari Kavu ya Kwala, mkoani Pwani ambayo itapunguza foleni ya malori ndani ya Jiji la Dar es Salaam.

Aidha, amewataka wasafirishaji kujiandaa kikamilifu kuitumia bandari hiyo, ili kupunguza msongamano na jitihada za serikali ni kuwaondolea kero wananchi na kuharakisha shughuli za kiuchumi.

Alisema ndani ya siku saba kuanzia Februari 2 hadi 8, mwaka huu, mchakato wa kuingia makubaliano na kampuni kubwa zitakazotumia bandari hiyo utaanza.

Prof. Kahyarara alisema hadi sasa jumla ya kampuni binafsi tisa zimeomba kupatiwa maeneo katika Bandari Kavu ya Kwala kwa ajili ya kuanzisha Container Freight Station (CFS), ili kuhudumia shehena ya madini ya shaba na mizigo mingine.

"Bandari ya Kwala ndio suluhisho la uhakika la kupunguza msongamano wa malori yanayoingia Dar es Salaam na kupitia Pwani," alisema.

Aidha, serikali imekamilisha taratibu zote ikiwamo kuweka maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na bandari na Bandari ya Kwala inatoa huduma zote.

"Mizigo yote itahudumiwa kwa njia ya treni kuelekea bandarini kutoka bandari kavu ya Kwala. Kwa kufanya hivyo serikali itaweza kupunguza foleni barabarani kuondoa msongamano bandarini na kuchochea matumizi ya reli katika kubeba mizigo.

Alizitaja bandari kavu nyingine zinazofanyiwa kazi ni Ihumwa Dodoma, Bahi Dodoma, Isaka Shinyanga na Fela Mwanza na kwamba mkakati ni kuzifanya kutoa huduma za kibandari ili kufupisha safari, pia kupunguza gharama na kuchochea matumizi ya reli.

# LATRA yakamilisha ukokotoaji nauli reli ya SGR Dar-Dodoma

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Usafiri Ardhini (LATRA), imesema inakamilisha upangaji wa viwango vya nauli ya Reli ya Kisasa (SGR), vitakavyokuwa vinatozwa baada ya kuanza rasmi kutoa huduma kwa treni ya mwendokasi kati ya Dar es Salaam na Dodoma.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, tayari Shirika la Reli Tanzania (TRC), lilishapendekeza viwango mbalimbali vya nauli za abiria kwa treni ya SGR na mamlaka hiyo imeitisha maoni ya wadau ili washiriki katika jambo hilo.

Suluo alisema mambo mengi ya kiufundi katika kuanza kwa huduma hiyo ya usafirishaji kwa njia ya reli ya kisasa yamekamilika na sasa wapo katika majaribio yanayotakiwa kufanyika kabla ya kuanza kutoa huduma kwa ajili ya usalama zaidi.

"Mfumo tayari umeshajengwa, mtu atatakiwa kuingia na kadi yake au kwa kutumia karatasi itakayokuwa imetoka kwenye mashine, hivyo tunaenda kukamilisha upangaji wa nauli ili ifikapo Julai, mwaka huu tuwe tumekamilisha," alisema Suluo. Alisema nauli za SGR zitakuwa zinatofautiana kutokana na madaraja.

"Kutakuwa na madaraja tofauti ikiwamo ya biashara na kiuchumi hivyo nauli ni lazima zitofautiane, baada ya kuwasili mabehewa tulikagua, tukataka TRC watuletee gharama za uwekezaji ili wasirudi tena serikalini kuomba uendeshwaji wa reli hii," alisema Suluo.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Senzige Kisenge, alisema yapo mambo mengi yanayotakiwa kufanyika kabla ya kuanza kutoa huduma ili kuhakikisha usalama wa huduma hiyo na kwamba kufanya majaribio kabla ya kuanza rasmi ni lazima.

Kisenge alisema majaribio wanayofanya ni kwa njia yenyewe pamoja na kichwa yanayofanywa kulingana na mpango waliojiwekea kwa msaada wa msimamizi.

Mwenyekiti wa Bodi ya LATRA, Prof. Ahmed Ame, alisema kuna haja ya LATRA kutambua ina jukumu kubwa katika usafiri huo kuliko ilivyo katika usafiri wa barabara kutokana na mradi huo kuhitaji usimamizi kwa umakini hususani kwenye utoaji wa huduma inayohusisha pia miundombinu na watoa huduma.

Tayari Rais Samia Suluhu Hassan ameshatoa maelekezo kwamba mpaka Julai, mwaka huu, treni hiyo inatakiwa iwe imeshaanza kutoa huduma ya usafirishaji kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma.

# Magari ya wagonjwa yakabidhiwa jimboni

**Na Munir Shemweta,** MLELE

MBUNGE wa Kavuu, Halmashauri ya Mpimbwe, Wilaya ya Mlele, mkoani Katavi na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda, amekabidhi magari mawili ya wagonjwa kwa halmashauri hiyo ili kusaidia kusafirisha wagonjwa.

Hafla ya kukabidhi magari hayo ilifanyika juzi katika Kituo cha Afya Isevya na kuhudhuriwa na viongozi wa halmashauri hiyo wakiwamo madiwani.

Wakati wa kukabidhi magari hayo, mbunge huyo alishukuru serikali kwa kuliwezesha jimbo lake kwa huduma za afya ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya na zahanati. "Nimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kusaidia ujenzi wa vituo katika jimbo langu, kwa kweli Mheshimiwa Rais ameifanya Mpimbwe kuwa na ustawi," alisema.

Mbunge Pinda aliitaka Halmashauri ya Mpimbwe na Kituo cha Afya Isevya kuhakikisha magari aliyoyakabidhi yanatunzwa vizuri na kutumika kwa yale malengo yaliyokusudiwa ya kutoa huduma kwa wananchi wa Mpimbwe.


## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA FEDHA

## MWALIKO KWA WADAU WA KUSHIRIKI KATIKA SHUGHULI ZA KAMATI YA MABORESHO YA SERA ZA KODI (TASK FORCE ON TAX REFORMS) KWA AJILI YA MATAYARISHO YA BAJETI YA 2024/25

Kamati ya Maboresho ya Sera za Kodi (Task Force on Tax Reforms) inayohusika na matayarisho ya Bajeti ya Serikali 2024/25 itaanza kazi yake mnamo mwezi Februari 2024. Vikao kazi vya Kamati vitazinduliwa na Kongamano la Kodi na Uwekezaji Kitaifa kwa mwaka 2024 ambalo litafanyika mwezi Februari.

Kila mwaka, Kamati hii, imekuwa ikipokea maoni ya wadau, kufanya uchambuzi, na kufanikisha majadiliano ya masuala mbalimbali yanayohusiana na sera za kodi na usimamizi wake. Maoni hayo yamekuwa na mchango mkubwa kwa waandaa sera na yamesaidia katika kuunda mfumo wa kodi ambao umewezesha utatuzi wa masuala mbalimbali ya kodi kwa ufasaha na uwazi.

Maboresho ya Sera za Kodi yanalenga kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuvutia uwekezaji; kuwezesha ukuaji wa biashara ndogondogo na za kati pamoja na ukuaji wa uchumi endelevu; kuboresha mazingira ya ulipaji kodi wa hiari; upanuzi wa wigo wa kodi na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika usimamizi wa kodi; kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi, kupunguza upotevu wa mapato, kuwianisha na kupunguza tozo na ada mbalimbali ili kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji.

Ili kufanikisha suala hilo, Kamati inakaribisha ushiriki wa Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi, Asasi zisizo za Serikali, Taasisi za Dini, Jamii ya Wasomi, Taasisi za Utafiti na Wataalamu wengine katika sekta ya uchumi kwa kutoa maoni ya kuboresha Sera za Kodi kwa maandishi. Vilevile, Kamati inakaribisha mada mbalimbali kutoka kwa wadau wanaopenda kufanya hivyo. Maoni na mada hizo zinapaswa kuonesha yafuatayo:-

i. Biashara, kampuni, taasisi, chama/vyama au makundi ambayo wanawakilisha;
ii. Mapendekezo ya mabadiliko ya kisera na mapato ya serikali yanayotokana na kodi na yasiyo ya kodi, ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa sekta, maeneo au aina ya walipakodi ambao wataathirika, na kwa namna watakavyoathirika;
iii. Makisio ya athari kwenye uchumi na mapato ya serikali katika mwaka huu wa utekelezaji na katika miaka ijayo;
iv. Sababu na uhalali wa mapendekezo ya mabadiliko kwenye sera za mapato, hususan uchambuzi wa namna ambavyo mapendekezo hayo yataisaidia Serikali kufanikisha malengo yake makuu ya kiuchumi, kodi na kupunguza umasikini; na
v. Pale ambapo mapendekezo yanapunguza mapato ya Serikali (hata katika kipindi cha muda mfupi), mapendekezo hayo hayana budi yaweke hatua bayana na za kuaminika sambamba na msukumo wa jumla wa sera za bajeti ya Serikali ili kufidia upungufu wa mapato ambao utajitokeza.

Tunatarajia kupata mapendekezo yatakayowezesha majadiliano yenye tija kati ya Serikali na Wadau.

Mapendekezo yawasilishwe kuanzia tarehe ya tangazo hili hadi tarehe 31 Machi 2024 kupitia lango (portal) lifuatalo: **https://maoni.mof.go.tz/**

**Kwa Nakala Ngumu tafadhali wasilisha kwa anuani ifuatayo:**
**Sekretariati ya Kamati ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi,**
**Wizara ya Fedha na Mipango,**
**Idara ya Uchambuzi wa Sera,**
**Jengo la Hazina (Ghorofa ya Pili),**
**18 Barabara ya Jakaya Kikwete,**
**S.L.P 2802,**
**DODOMA.**

Barua Pepe: mathias.kadebe@hazina.go.tz au salha.mzee@hazina.go.tz

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Mathias Kadebe **0713 694 895; au Salha Mzee 0652 442 944.** Pia tembelea tovuti yetu: **www.mof.go.tz.**

**Tangazo hili limetolewa na:**

**Dkt. Natu E. Mwamba**
**Februari 2024**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi Ligi Kuu chezesheni kwa haki tuwaone AFCON 2025

**ILIPOTOKA** orodha ya waamuzi watakaochezesha Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, inayoendelea nchini Ivory Coast bila kuwamo hata mmoja kutoka Tanzania, ilileta mjadala mkubwa sana.

Kwenye redio, televisheni, vijiwe vya kahawa na mitandao ya kijamii kulichafuka kwa mijadala mbalimbali kuhusu kwa nini hakuna mwamuzi hata mmoja tu aliyejumuishwa kwenda kuchezesha fainali hizo ambazo kwa sasa zipo hatua ya nusu fainali.

Kilichowachefua mashabiki wengi wa soka nchini ni kuona hata baadhi ya nchi ambazo ni majirani zetu na zingine hazina rekodi nzuri, tena timu zao za taifa hazikufuzu fainali hizo, lakini zilitoa waamuzi.

Mfano Ndabihawenimana Pacifique kutoka Burundi, Peter Waweru wa Kenya, Uwikunda Samuel kutoka Rwanda, Omar Abdulkadir Artan wa Somalia na Mahmood Ali wa Sudan.

Ukitazama vizuri hapa, hawa wanatoka kwenye Ukanda wa CECAFA na timu za taifa hazijafuzu, lakini wenyewe wamechaguliwa kwenda kuchezesha, iweje Tanzania ambayo timu yao imefuzu ila imekosa mwamuzi?

Tumekuwa tukiwasema wachezaji wetu kuwa wajifunze kutoka kwa wenzao wa nje, lakini kinachoonekana ni kwamba Stars tayari wameshajifunza na ndiyo maana wamekwenda AFCON, imefikia wakati sasa kuwageukia waamuzi nao wajifunze kutoka kwa wenzao kutoka mataifa haya haya jirani ya CECAFA, kama Somalia, Rwanda, Kenya na Burundi.

Kwani waamuzi hawa waliochaguliwa wana nini? Na waamuzi wa Tanzania wanashindwa kwa nini? Inawezekana Kamati ya Waamuzi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), wana kitu wanachokijua kuhusu waamuzi wa Tanzania ambacho sisi hatukijui?

Naamini baadhi wanakijua ila wamekuwa wanakifumbia macho. Ni wazi baadhi ya waamuzi wetu wameonekana kutokuwa makini katika vitu vingi, kama vile utimamu wa mwili, kutafsiri sheria, kufanya maamuzi magumu na wakati mwingine kutoaminika pia.

Unaweza ukajiuliza mbona hata waamuzi wanaochezesha AFCON wanaonekana kuna baadhi ya matukio inabidi wasaidiwe na mashine za VAR? Ni kweli, lakini ukiangalia matukio hayo yanakuwa machache na maneno ya maamuzi ya mwisho tu.

Ukiacha hayo wenyewe wapo fiti, na wana uwezo mkubwa wa kutafsiri sheria na kuiacha mechi kujiamua yenyewe bila kuwa na maamuzi mengi yenye utata. Tukumbuke kuwa hata waamuzi waliochaguliwa huko kwenye ligi zao hakuna VAR, lakini uchezeshaji wao bora ndiyo umewafanya wachaguliwe, mengine yanakuwa ziada tu.

Kwa sasa Ligi Kuu Tanzania Bara imerejea, hivyo waamuzi wanaweza kuanza kuwa makini kwa sababu watakuwa wamepata somo kutoka AFCON inayoendelea kwa Timu za Taifa za Afrika Kusini, DR Congo, Nigeria na mwenyeji, Ivory Coast kutinga nusu fainali.

Kuchezesha kwa haki katika mechi za Ligi Kuu ndiko kutawafanya kuangaliwa kwa jicho la tatu na kamati itakayochagua waamuzi wa kwenda kuchezesha fainali za AFCON 2025 zitakazofanyika nchini Morocco. Waamuzi wetu wasiridhike tu na kuchezesha mechi za Ligi Kuu, badala yake wawe na wivu na wenzao ambao wanachezesha fainali hizo, wakiwa katikati ya wachezaji wakubwa barani Afrika na Ulaya kwa ujumla.

Kuendelea kuchezesha kwa bora liende, upendeleo, rushwa, kutojiamini, au mapenzi kutawafanya kubaki hapa hapa na kutopiga hatua katika maendeleo yoyote kwake mwenyewe na kuikosesha sifa nchi. Tunaamini kwa michuano hii ya Afcon 2023, sasa somo limeeleweka, hivyo tunatarajia mechi nyingi za Ligi Kuu zimalizike bila malalamiko yoyote makubwa ya msingi ili mwaka 2025 kuwe na waamuzi kutoka Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Hongera TPLB, kupunguza wageni ni uvivu wa kufikiri

**WAKATI** akiwapongeza wachezaji walioiwakilisha Ligi Kuu ya Tanzania Bara kwenye Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, zinazoendelea nchini Ivory Coast, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi nchini (TPLB), Almasi Kasongo, alibainisha kuwa yeye si muumini wa kupunguza wachezaji wa kigeni ili wachezaji wa Kitanzania wapate nafasi.

Akasema anaamini uwezo wa wachezaji hao unawapa fursa kujifunza na kuwa bora zaidi.

"Mimi siku zote mtazamo wangu vijana wa Kitanzania wakipata nafasi, msingi mkubwa ni kujituma, nidhamu, kupambana na kusikiliza yale ambayo walimu wanawaambia, binafsi sijawahi kuwa muumini kuonyesha kuwa ukiwa na wachezaji wengi wa kigeni katika ligi yako tafsiri yake ni kwamba eti wachezaji wako wa ndani wanakosa nafasi ya ushindani," akasema.

Alisema hayo siku akiwapongeza Henock Inonga wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Djigui Diarra wa Mali ambao timu zao za taifa zilifanikiwa kuingia robo fainali ya michuano hiyo.

Wachezaji hao wote wanachezaji Ligi Kuu Tanzania Bara, Diarra akiichezea Yanga kama kipa namba moja, na Inonga akiwa beki wa kutegemewa Simba.

Mbali na kusema hayo, Kasongo alibainisha inaonyesha kuwa Ligi Kuu Tanzania Bara imepiga hatua na imedhihirisha kile ambacho awali walikuwa wanahitaji, klabu kusajili wachezaji wa kigeni angalau wanaocheza timu za taifa na wenye uwezo mkubwa kitu ambacho sasa kimeonyesha mafanikio.

"Ile mijadala iliyokuwa inaanzishwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari na kuchagiwa kwa muda mrefu na sisi kuweka kanuni matunda yake yanaanza kuonekana kwamba klabu zimeanza kutuletea wachezaji ambao wanaendana na ubora wa ligi yetu, wanaozisaidia klabu zao na kuzibeba timu zao za taifa, ni jambo kubwa kwa Bodi, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) na mpira wa Tanzania," akasema.

Kwa sasa Ligi ya Tanzania imebakiwa na mchezaji mmoja tu, Inonga baada ya Diarra kuondolewa juzi na wenyeji Ivory Coast, timu yake Mali ikifungwa mabao 2-1. AFCON ya mwaka huu ilikuwa na wachezaji 19, wageni na wenyeji wanaocheza Ligi Kuu ya Tanzania.

Na hii imesababisha mwaka huu kuwa na msisimko mkubwa nchini, hasa kwenye vibanda umiza kwani licha ya Stars kuwamo, lakini mashabiki wamekuwa wakijazana kwenda kuangalia na kuwashangilia wachezaji wa klabu zao wanaowakilisha timu zao za taifa.

Nimpongeze sana Kasongo kwa hili, kwani kwa miaka mingi kumekuwa na dhana kuwapo kwa wachezaji wengi wa kigeni kwenye Ligi Kuu ya Tanzania kunawanyima nafasi wachezaji wazawa.

Pamoja na kwamba huenda ukawa ni mtazamo wake na si wa Bodi ya Ligi, lakini hili linaonyesha kuwa wapo baadhi ya viongozi wanaujua ukweli na wanaweza kuutekeleza na kuusimamia kwenye vikao vyao.

Wachezaji wa kigeni pamoja na kuzipaisha sana Klabu za Simba na Yanga kwenye michuano ya kimataifa, lakini safari hii tumeona faida nyingine nayo ni kuitangaza Ligi Kuu ya Tanzania.

Diarra ndiye kipa namba moja kwa sasa wa Mali, akikaa mechi zote dhidi ya makipa wengine wanaocheza soka nje ya Afrika.

Hii ni sifa na fahari kwa soka la nchi nzima kwani hata klabu wanazocheza makipa hao watataka kuangalia ligi inayotoa kipa bora kwenye kikosi cha timu ya taifa mpaka makipa wao wanakaa benchi.

Tunaona Inonga ameanza kunyemelewa na klabu nyingi ndani na nje ya bara la Afrika kutokana na uwezo mkubwa aliouonyesha kwenye fainali hizo.

Amekuwa bora zaidi na tegemeo la nchi yake kuliko hata mabeki wengine wa Kikongomani wanaocheza soka la kulipwa barani Ulaya. Hapa ndipo utakapoona umuhimu wa wachezaji wa nje kwenye klabu za Tanzania, hivyo badala ya kuwazuia ili wachezaji wa Tanzania wapate urahisi wanatakiwa waje ili wa hapa wajifunze.

Ukiangalia hata wachezaji wa Kitanzania wanaoichezea Stars wanaotoka kwenye klabu za Ligi Kuu, ni wale waliojipenyeza, kupambana na kupigania namba na wageni kama kina Kibu Denis, Mzamiru Yassin, Aishi Manula, Mohamed Hussein kwa upande wa Simba, Ibrahim Hamad 'Bacca', Dickson Job, Bakari Mwanyeto, Mudathir Yahaya kwa upande wa Yanga. Nadhani imefika wakati tuache wachezaji wetu wapambane wenyewe kusaka namba ili kuwafanya na wao wawe bora mbele ya wachezaji wa kigeni kwa faida ya pande zote mbili, mpira wa Tanzania, ubora wa Ligi Kuu na wachezaji wenyewe.

Siasa iachwe ili soka la ukweli lichezwe, mwenye uwezo ataonekana hata kama akicheza na Ronaldo au Messi. Nimemwelewa Kasongo na kwa hili 'kaka' chukua kongole yako.

# Wajivunia kupata faida ya bil. 92.2/-

**Na Halfani Chusi**

BENKI ya Exim imetangaza ripoti yake ya kifedha kwa mwaka 2023, ikionesha mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali ikiwamo ongezeko la faida kabla ya kodi kwa asilimia 36 kutoka Sh. bilioni 67.8 mwaka 2022 hadi Sh. bilioni 92.2 mwaka 2023.

Ikiashiria maendeleo mazuri ya benki hiyo, ripoti hiyo imeonesha ongezeko la asilimia sita kwenye Mapato ya Jumla (Total Revenue) ambayo yalipanda kutoka Sh. bilioni 236.7 mwaka 2022 hadi Sh. bilioni 251.2 mwaka 2023.

Akizungumzia taarifa hiyo mwishoni mwa wiki, Ofisa Mkuu wa Fedha wa benki hiyo, Shani Kinswaga, alisema mafanikio hayo yanadhihirisha uimara wa benki hiyo sokoni na zaidi unasisitiza azma yake thabiti katika utoaji huduma bora za kibenki.

"Ukuaji huu wa faida kipekee unawakilisha azma yetu ya kutoa huduma bora na uwezo wetu wa kuongeza thamani kwa wadau wetu wakiwamo wateja wetu.

"Mafanikio haya ni matokeo ya mkakati wetu katika kuongeza zaidi vyanzo vya mapato na kuongeza ufanisi katika uendeshaji wa taasisi hii," alisema Kinswaga.

Zaidi, kupitia ripoti hiyo, Benki ya Exim imeshuhudia ongezeko kubwa la Amana za Wateja kutoka Sh. trilioni 1.8 mwaka 2022 hadi Sh. trilioni 2.4 mwaka 2023, ikiwa ni ongezeko la asilimia 32. "Ongezeko la Amana hizi linathibitisha sifa ya Exim katika utoaji wa huduma za kibenki zenye kuaminika na zenye uaminifu kwa wateja wetu tunaowathamini," aliongeza Kinswaga.

Alieleza jitihada za benki hiyo katika kusaidia sekta mbalimbali za uchumi na kukuza maendeleo endelevu nchini zimezaa matunda kwa kuwa mikopo na kiwango cha utoaji mikopo hiyo kiliongezeka kutoka kiasi cha Sh. trilioni 1.2 mwaka 2022 hadi Sh. trilioni 1.5 mwaka 2023, ikiwakilisha ongezeko lenye kuridhisha la asilimia 22.

Kwa upande wa mali, Exim ilishuhudia ukuaji mkubwa katika jumla ya mali zake kutoka thamani ya Sh. trilioni 2.4 mwaka 2022 hadi Sh. trilioni tatu mwaka 2023, ikiashiria ukuaji wa asilimia 26.

Mafanikio haya yanatajwa kuwa yanaimarisha zaidi msimamo wa kifedha wa benki hiyo na hivyo kuthibitisha uwezo wake imara kwenye uendeshaji shughuli zake.

"Hisa za wanahisa wetu ziliongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka Sh. bilioni 264.5 mwaka 2022 hadi Sh. bilioni 313.7 mwaka 2023, likiwa ni ongezeko la asilimia 19.

"Mafanikio haya yanadhihirisha imani na uaminifu ambao wanahisa wetu wanao kutokana na mwelekeo na usimamizi wetu," aliongeza Kinswaga.

Zaidi ya mafanikio yake ya kifedha, katika kipindi cha mwaka 2023, Exim iliendelea kuwekeza zaidi jitihada zake katika eneo zima la uwajibikaji kwa jamii (CSR) ikiongozwa na mpango wake endelevu unaofahamika kama Exim Cares.

Uwekezaji wa benki hiyo na uungaji mkono wa miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ulichangia kuongeza kasi katika maendeleo ya nyanja hizo muhimu nchini ikiwamo sekta ya afya, mazingira na kuwajengea uwezo wajasiriamali hususani wanawake.

Kwa upande wa miundombinu, katika kipindi cha mwaka huo, benki hiyo iliboresha mfumo wake mkuu wa huduma za kibenki ikilenga kutoa huduma bora zaidi kwa wateja wake.

Mfumo huo mpya ulilenga kurahisisha uchakataji miamala, kuongeza usalama, kutoa huduma za kibenki bila vikwazo ili kuwawezesha wateja kufurahia huduma za kifedha kwa urahisi na utulivu.

"Hatua hiyo muhimu inathibitisha azma yetu ya kutoa huduma zaidi ya mazoea ya kawaida katika utoaji huduma za kibenki," alisema.

Kufuatia mafanikio hayo, Kinswaga alielekeza shukrani zake kwa wafanyakazi, wateja na wanahisa wa benki hiyo akisema, "ushirikiano wetu wa pamoja, pamoja na azma yetu ya ubunifu, uzingatiaji wa mahitaji ya wateja, na ufanisi wetu kwenye utoaji wa huduma zetu vimekuwa ndio msingi wa mafanikio yetu.

"Tutaendelea kuweka kipaumbele zaidi kwenye maeneo haya ili kuchochea ukuaji endelevu na kuunda thamani ya muda mrefu kwa wadau wote."



Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Batista Kashusha (wa pili kulia), akisoma taarifa ya Mahakama hiyo katika Siku ya Sheria iliyofanyika mwishoni mwa wiki, wa pili kushoto ni Mkuu wa Wilaya, Loutery Kanoni, aliyekuwa mgeni rasmi katika sherehe hizo. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Waziri atoa siku 14 malalamiko walimu 136,000 yashughulikiwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ametoa siku 14 kwa maofisa utumishi wa halmashauri kufanya uhakiki wa kina wa taarifa za watumishi kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) ili kushughulikia malalamiko ya walimu 136,000 yaliyobainika. Mohamed Mchengerwa aliagiza hayo jana jijini Dodoma wakati wa kikao kazi cha Maofisa Utumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali wanaohakiki kwa kina changamoto za walimu hususan upandishwaji vyeo.

Alisema katika kuhakikisha malalamiko ya walimu yanashughulikiwa, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Utumishi iliagiza Tume ya Utumishi wa Walimu kufanya uchambuzi na kubaini walimu wote wenye changamoto katika upandaji wao wa vyeo.

"Niwapongeze watendaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ambapo uchambuzi umefanyika na walimu zaidi ya 136,000 wamebainishwa kuwa na changamoto.

"Pamoja na kazi nzuri iliyofanyika, kwa kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa malalamiko ya walimu wote yanashughulikiwa kwa ufanisi, nimeelekeza uhakiki wa kina ufanyike kwa kuhusisha taarifa za watumishi kama zilivyo kwenye mfumo wa HCMIS," alisema.

Aliagiza kushughulikiwa kikamilifu malalamiko hayo ndani ya siku 14 kwa ufanisi wa hali ya juu ili kuhakikisha hakuna mwalimu anayeachwa baada ya uhakiki huo.

"Ninaomba niweke wazi, mimi sitamvumilia mtendaji yeyote ambaye hawajibiki kushughulikia kero za walimu na vilevile sitamani kusikia walimu wana malalamiko kuhusu maslahi yao ya kiutumishi.

"Rais anataka kila mmoja wetu katika wizara hii TAMISEMI kufuatilia kwa msingi haki za kila mwalimu, kupekua, kutafuta na kushughulikia," aliagiza.

Alisema kuwa hata kwa walimu wanaoumwa (wako kitandani) na wenye dharura za ugonjwa, haki zao zishughulikiwe ili kurekebisha kasoro zilizokuwapo na kuwaweka walimu wote nchini katika usawa.


Waziri Mchengerwa aliagiza wakurugenzi ambao hawajawalipa maofisa utumishi wao hadi kufikia leo wawe wamelipa stahiki zao.

"Katibu Mkuu ikifika hadi saa 12 jioni Jumatatu niletee orodha ya wakurugenzi ambao hawajawalipa stahiki zao maofisa utumishi ili nichukue hatua mara moja.

"Ninatarajia mtakuwa makini na kufanya kazi hii kwa ufanisi ili kuhakikisha hakuna mwalimu atakayeachwa baada ya zoezi hili kufanyika," aliagiza.

Awali Naibu Katibu Mkuu katika ofisi hiyo anayeshughulikia elimu, Dk. Charles Msonde, alisema Tume ya Utumishi wa Walimu imefanya uchambuzi na kubaini walimu wenye changamoto katika upandaji wa vyeo ni zaidi ya walimu 136,000.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed





Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ustawi na Maendeleo ya Jamii wakitembelea mradi wa kiwanda cha sukari Mkulazi, mkoani Morogoro juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

KIWANDA CHA SUKARI MKULAZI

# Kamati ya Bunge yaridhishwa, chaanza uzalishaji kikitoa ajira kwa wananchi

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Fatma Taufiq, amesema wajumbe wa kamati hiyo wamefurahishwa na kukamilika kwa kiwanda cha uzalishaji sukari cha Mkulazi kilichoko mkoani Morogoro.

Aliyasema hayo juzi wakati kamati hiyo ilipofanya ziara ya kutembelea kiwanda hicho na kukuta kimeshaanza uzalishaji sukari.

Fatma alisema tayari kiwanda hicho kimeanza uzalishaji sukari, kikianza kuzalisha tani 320 huku matarajio yakiwa kuzalisha tani 50,000 kwa mwaka.

Alipongeza serikali kwa kuruhusu ujenzi wa kiwanda kuendelea. Kiwanda kilianza kujengwa mwaka 2016 chini ya ubia baina ya NSSF na Jeshi la Magereza.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alisema kiwanda hicho kina faida kubwa kwa taifa ikiwamo kuzalisha ajira kwa wananchi, uzalishaji umeme zaidi ya megawati 15 ambapo megawati saba zinakwenda kuingia katika Gridi ya Taifa kwa maana kiwanda kitauza umeme huo.

"Tunamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kufanyia kazi changamoto ya sukari kupitia mradi huu ambao unakwenda kupunguza tatizo la sukari," alisema.

Naibu Waziri Katambi alisema wizara inafurahishwa na uwekezaji uliofanyika. Wanapenda kuona miradi kama hiyo inayogusa wananchi na Watanzania wote inakuwa mingi.

"Mradi huo una kubwa na umezalisha ajira za kutosha. Miradi kama hii ndio Mheshimiwa Rais anataka na ndio itakayotufanya tuwe wa tofauti," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, alisema mradi huo unamilikiwa kwa ubia baina ya NSSF na Jeshi la Magereza. NSSF inamiliki asilimia 96 na Jeshi la Magereza asilimia nne.

"Kwetu sisi NSSF ni faraja kubwa kufikia hatua hii kwa sababu ndio lengo la mfuko kuwekeza katika kiwanda hiki ambacho tunaamini pasi na shaka kitarudisha fedha zilizowekezwa," alisema Mshomba.

Alishukuru wajumbe wa kamati hiyo ya Bunge kwa ushauri wao wa mara kwa mara, pia wizara na viongozi wake kwa ushauri wao katika utekelezaji mradi huo.

"Kwa kweli msaada kutoka wizarani na viongozi wa serikalini pamoja na kamati umetusaidia sana kuona ya kwamba tunafika mahala pazuri na kiwanda kimeanza uzalishaji," alisema.

Aliongeza: Tayari ripoti kutoka kwa wataalamu zinaonesha uwekezaji wote utakuwa umesharejeshwa katika kipindi kisichozidi miaka minne na nusu, huu ni mradi mkubwa sana na wenye manufaa makubwa sana kwa watu wote, yaani wananchi kwa ujumla na serikali."

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni Hodhi ya Mkulazi, Dk. Hildelitha Msita aliishukuru kamati hiyo kwa kutembelea mradi huo na kutoa ushirikiano wa kuboresha mradi huo.

Kamishna Msaidizi wa Magereza, Majungu Liro, alisema Jeshi la Magereza ni mojawapo ya wabia katika mradi huo mkubwa, ambao umeongeza ajira kwa wananchi.

"Pamoja na kwamba sisi ni wabia katika mradi huu, sisi ndio tunahusika na ulinzi wa kiwanda hiki kwa asilimia 100," Kamishna Msaidizi Liro alisema.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo ya Bunge, wakiwamo Boniphace Getere, Almas Maige na Neema Lugangira, walipongeza serikali kwa kazi kubwa iliyofanyika kiwandani huko na wamefurahi kuona kiwanda kimeanza uzalishaji sukari.

Selestine Some, Mtendaji Mkuu wa Mkulazi, alisema ujenzi wa kiwanda hicho ulianza Julai 2016 na ilipofika tarehe 28 Novemba 2023, walianza uzalishaji sukari kwa majaribio.

Alisema kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 50,000 kwa mwaka. Mpaka sasa mradi umetoa ajira kwa wananchi 2,020 ambazo ni ajira za moja kwa moja huku zaidi ya watu 8,000 wakinufaika na mradi huo.

# UNFPA yapewa mil. 921/- kutekeleza mradi afya ya mama na mtoto Kigoma

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI ya Japan imetoa Sh. milioni 921 kwa ajili ya kusaidia kuendeleza mradi wa afya ya mama na mtoto kwenye kambi za wakimbizi za Nyarugusu na Nduta mkoani Kigoma.

Mradi huo wa mwaka mmoja unaoratibiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, unahusisha pia maeneo ya jirani na kambi hizo katika wilaya za Kibondo na Kasulu.

Baada ya kutia saini makubaliano ya utekelezaji mradi huo jijini Dar es Salaam juzi, Balozi wa Japan nchini, Yasushi Misawa alisema nchi yake imejikita kusaidia sekta nyingi nchini.

"Ushirikiano wa Japan na Tanzania umejikita katika sekta nyingi; afya, kilimo, miundombinu mbalimbali, utawala bora, viwanda na nyingine. Hata fedha tulizotoa ni sehemu ya ushirikiano huo," Balozi Miswa alisema.

Balozi huyo alisema huduma za afya ni moja ya vipaumbele vya ushirikiano wa nchi hizo mbili. Programu ya afya ya mama na mtoto mkoani Kigoma ni sehemu ya ushirikiano huo.

Aliipongeza Serikali ya Tanzania kwa juhudi zake za kuboresha huduma za afya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa afya ikiwamo kujenga zahanati na vituo vingi vya afya.

Mwakilishi Mkazi wa UNFPA Tanzania, Mark Bryan Schreiner, alisema watanunua gari maalum la kuratibu shughuli za afya ya uzazi katika eneo hilo na kutoa mafunzo kwa madaktari 25 na wauguzi 25 wanaofanya kazi katika kambi hizo na maeneo ya jirani.

Schreiner alisema katika mradi huo, watumishi 15 wa afya watapata ajira kwa ajili kutoa huduma kwa wakimbizi na watu wanaoishi karibu na kambi hizo.

"Katika utekelezaji mradi huu, kutakuwa wa utoaji elimu ya afya ya uzazi kwa wakimbizi na wakazi wa maeneo yanayozunguka kambi hizo," alisema.

Schreiner alisema walengwa wakuu wa elimu hiyo ni mabinti wanaopata mimba za utotoni ili wawe na uelewa wa kutosha kuhusu madhara yatokanayo na mimba hizo.

Alibainisha kuwa wanawake na wasichana 3,000 kutoka kambi za Nyarugusu na Nduta na wakazi 3,000 wanaoishi karibu na kambi hizo, pia watapewa taulo za kike ndani ya kipindi cha mwaka mmoja.

"Mradi huu pia utanufaisha zaidi ya watu 113,000 wakiwamo wanawake, wasichana, waliojifungua wakiwa na umri mdogo, wavulana waliobalehe na watu wenye ulemavu walioko nje na ndani ya kambi za wakimbizi," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Majaliwa Marwa, ofisa wa UNFPA, hadi Disemba 31, mwaka jana, Kambi ya Wakimbizi Nyarugusu ilikuwa na wakimbizi 136,478 huku Kambi ya Nduta ikiwa nao 64,010.

Ofisa huyo alibainisha kuwa wakimbizi wapya walioingia katika Kambi ya Nyarugusu kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) mwaka huu ni 14,540. Kati yao, wanawake ni asilimia 56.



## HABARI KASKAZINI

# Serikali yaita wawekezaji nishati jadidifu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imewaalika wawekezaji wakubwa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika miradi ya kuzalisha nishati jadilifu kwa kutumia vyanzo mbadala ikiwamo gesi, upepo, jua na joto ardhi ili kuongeza uzalishaji na kutatua changamoto ya upungufu wa umeme.

Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), John Mageni, aliyasema hayo jijini Arusha, katika mkutano wa tano wa ushirikiano wa nishati Tanzania ulioandaliwa na EnergyNet.

"Tumekuja kukutana na wadau wa nishati katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika na tunakutana na wawekezaji wenye nia ya kuwekeza nchini katika maeneo haya, pia tumekutana na timu ya watu wanaohusika kutoa fedha katika miradi ya nishati kwa ajili ya kuboresha hali ya upatikanaji umeme nchini," alisema.

Alisema katika mkutano huo, walishawishi uwekezaji katika nishati jadilifu hasa upande wa jua na upepo kwa kuwa miradi iliyopo ni midogo na imejikita maeneo ya vijijini.

Alisema kazi wanayoifanya ni kushawishi sekta binafsi, kuwekeza katika miradi mikubwa inayoanzishwa ya uzalishaji wa Megawati 100 hadi 200 na kuendelea ili kuwa na nishati mbadala katika mfumo wao.

"Sehemu kubwa ya uzalishaji wa nishati yetu ni gesi na maji na inapotokea changamoto katika vyanzo hivyo athari zake zinakua za moja kwa moja na kwa sasa kama nchi tumeamua kuingia katika vyanzo vingine mbadala vya nishati jadilifu," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali imefanya jitihada mbalimbali na tayari kuna kampuni kubwa tano zinakamilisha utaratibu wa ujenzi wa miradi mikubwa kwenye nishati jadilifu ambazo zikianza uzalishaji zitawezesha kupata megawati 700 za umeme katika mfumo wa Gridi ya Taifa.

Mkutano huo uliwakutanisha wadau na wakuu wa sekta ya nishati kutoka nchi za ukanda wa Afrika Mashariki (EAC) na Kusini mwa Afrika yenye azimio la kutumia vyanzo mbadala vya umeme, badala ya kutegemea maji na gesi ambavyo wakati mwingine kunakuwa na ukame na kusababisha upungufu.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba (kushoto), akisisitiza jambo kuhusu bei elekezi ya sukari kwa mfanyabiashara, Latifa Shehoza (katikati), anayeuza bidhaa kwa bei ya jumla, wakati wa ziara yake sokoni hapo juzi Barabara ya 11 jijini Tanga. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# RC atoa chakula kituo cha yatima

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, ametoa msaada wa vyakula na mahitaji mengine muhimu kwa watoto yatima wanaoishi kwenye makazi ya The Joy of God Ophanance yaliyoko jijini Arusha.

Msaada huo umetolewa kupitia fedha walizozawadiwa na watumishi wa Sekretarieti Mkoa wa Arusha, wakati wa sherehe za kuukaribisha mwaka mpya wa 2024.

Msaada huo ni ahadi aliyoitoa siku ya sherehe ya kukaribisha mwaka 2024, baada ya watumishi wa sekretarieti mkoa huo, kuwazawadia fedha yeye na Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Missaile Albano, pamoja na Katibu Tawala Msaidizi Utawala na Rasilimali Watu, David Lyamungi. "Tunawashukuru watumishi wote kwa zawadi hii mliyotupatia, tunaithamini na kutambua umuhimu wake, fedha hizi tutanunua chakula na kupeleka kwa watoto yatima wa Kituo cha The Joy of God kwa kuwa amenipigia simu kuwa wana uhitaji wa chakula katika kituo hicho," alisema Mongella.

Akizungumza mwisho wa wiki baada ya kupokea chakula hicho, Msimamizi wa kituo hicho, Mtawa Janeth Ngopa, alisema zawadi ya chakula kwa watoto hao ina thamani kubwa.

Aliongeza kuwa uwepo wa chakula cha kutosha kituoni hapo, utawahakikishia afya watoto hao pamoja na kuwafanya kuwa na furaha na matumaini wakati wote.

"Tunakushukuru Mheshimiwa Mongella kwa upendo wako kwetu na moyo wa kutoa, tunakuombea kwa Mungu azidi kumbariki, kupitia kwa watoto hawa wanafarajika hata sisi walezi tunakuwa na amani," alisema. Hata hivyo alisema watoto hao wamemshukuru kiongozi huyo kwa kuwajali na kujitoa mara zote bila kuchoka, kwa kuwa amekuwa akiwatembelea mara kwa mara na kuwapa mahitaji mbalimbali na aliahidi wataendelea kumwombea baraka kutoka kwa Mungu.

"Kupitia chakula hiki tunamwombea mkuu wa mkoa ili Mungu ampe maisha marefu na azidi kumbariki kwa kumzidishia mara dufu pale alipotoa kwa ajili yetu," alisema.

Awali, vyakula vilivyokabidhiwa ni pamoja na kilogramu 150 za mchele, kilogramu 65 za unga wa mahindi, kilogramu 100 na kilogramu 50 za maharagwe vyenye thamani ya Sh. 822,000.

# RIVACU kumwangukia PM mgogoro wa shamba

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKUTANO Mkuu Maalum wa Chama Kikuu cha Ushirika (RIVACU) mkoani Manyara, umeazimia kwenda kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kumlilia awasaidie wasinyang'anywe mashamba yao ya ushirika yanayotishiwa kufutwa na viongozi wa serikali.

Katika kuhakikisha kuwa suala hilo linafanikiwa chama hicho kimeunda kikosi kazi cha timu ya watu sita ambao watakutana na Waziri Mkuu kumwangukia kuhusu suala hilo.

Azimio hilo lilifikiwa mwishoni mwa wiki iliyopita na wajumbe wa mkutano mkuu maalumu baada ya kujadiliana takribani saa nne Mjini Babati juu ya namna viongozi wa serikali wanavyotumia mashamba yao kisiasa.

Azimio jingine walilolipitisha ni kuhakikisha ekari 2020 za shamba la Dareda haziguswi na mvamizi yeyote na kutokuridhia kufutwa kwa shamba hilo na mashamba mengine.

Maazimio hayo yalisomwa mwisho wa wiki na Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu maalumu Patrick Sulley, baada ya kujadiliana kwa muda mrefu.

Sulley alisema wameamua hivyo baada ya kuona mashamba yao yanaendelea kupokonywa na wananchi na viongozi wa serikali wakishinikiza yafutwe bila kutoa sababu za msingi licha ya RIVACU kuridhia kuwamegea ardhi wananchi walipovamia.

Alisema wameamua kwenda kwa Waziri Mkuu kwa kuwa walishakwenda mara mbili kwa Waziri wa Kilimo ila hawaoni hatua zikichukuliwa.

Alisema ikiwa Waziri Mkuu atashindwa kuwasaidia watakimbilia Chama cha Mapinduzi (CCM) makao makuu kumlilia Katibu Mkuu, Dk.Emmanuel Nchimbi.

Awali Mwenyekiti wa RIVACU, Yuda Sulley, alisema nia yao ni kwenda kumuona Waziri Mkuu kipindi cha Bunge lililoanza wiki iliyopita ambapo walishaongea na Mbunge wa Hanang', Samweli Hhayuma akawaahidi kuwasaidia kuwakutanisha na Majaliwa.

Alisema watakapomwona watazungumzia shamba la Dareda, Shamba la Mwada, Shamba la VIPIN lililopo Wilaya ya Karatu ambapo kuna wanachama wao, Shamba la Mbulu na Hanang'.

Pia Michael Tsaxara alisema ushirika siyo bahati mbaya na siyo gongo hivyo wang'ang'anie ekari 2020 zisipungue katika Shamba la Dareda.

Naye Ofisa Sheria Tume ya Maendeleo ya Ushirika kutoka Makao Makuu, Donald Deogratius, aliwasihi wajipange ili hata watakapoulizwa maswali kuhusu mgogoro huo wawe na majibu yatakayosaidia kuleta utatuzi.

Mwanasheria huyo alisema Rais anapoamua kuchukua ardhi yeyote kwa matumizi lazima atoe fidia.





# Tumbaku yaongoza kuingiza mapato Ushetu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

LICHA ya kutopewa kipaumbele zao la tumbaku limeongoza kuiingizia mapato kwa asilimia zaidi ya 69 Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu katika makusanyo ya nusu ya mwaka wa fedha 2023/24 katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2023.

Katika kipindi hicho, tumbaku imetajwa kuchangia Sh.bilioni 2.028 kati ya Sh.bilioni tatu fedha za mapato ya ndani iliyokusanywa ambapo walifikia asilimia 104 ya makadirio.

Kwa mujibu wa Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, Shigela Ganja, mazao yaliyofuatia kwa ukusanyaji ni pamba Sh.milioni 121.1, mpunga milioni 58, mahindi milioni 85, alizeti milioni tano na mazao mengine mchanganyiko yakichangia Sh.milioni 140.

Ganja alisema makadirio ya halmashauri hiyo yalikuwa ni kukusanya Sh.bilioni tatu nyuma ya kile kilichopatikana na kutaja mifumo rafiki ya ukusanyaji kuwezesha kupita makadirio hayo.

Baadhi ya wakulima wa zao hilo walisema limekuwa halipewi kipaumbele ikiwamo kutotengewa fedha zinapotengwa bajeti kwa ajili ya kilimo tofauti na mazao mengine ambayo yamekuwa yakitengewa fedha kwa ajili ya pembejeo.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Hadija Kabojela, alisema bajeti ni shirikishi ilianzia kwa wananchi kuainisha vipaumbele vyao na mahitaji hivyo hakuna sehemu inayopendelewa bali ni kutokana na mahitaji ya wananchi.

Pia alisema fedha zinazopatikana watahakikisha wanaipata nafasi miradi yote iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi hasa kwenye sekta ya afya na elimu.

Alisema, walipokea zaidi ya Sh.bilioni 6.5 sawa na asilimia 55 ya bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kuanzia mwezi Julai hadi Desemaba huku ruzuku ikiwa ni Sh.bilioni 1.1, serikali kuu na wafadhili Sh.bilioni 5.4.

Alisema, mpaka sasa miradi yote iliyokuwa kwenye mipango imekamilika ambapo ni matundu 66 ya vyoo kwenye shule za msingi kumi ,ukamilishaji wa jengo la mama na mtoto kituo cha afya Igwamanoni na ujenzi wa sekondari moja Kata ya Ulowa.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mdeme, akizungumza katika kusherehekea Siku ya Polisi pamoja na familia zao mkoani humo iliyofanyika katika Viwanja vya Polisi Kambarage Manispaa ya Shinyanga juzi. **PICHA: SIMON KAMGISHA**

# Mvua yakata barabara Kaliua

**Na Vitus Audax**

MVUA inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali mkoani Tabora imesababisha mawasiliano ya barabara katika Kijiji cha Imaraupina, Kata ya Ushokola, wilayani Kaliua kukatika hali iliyosababisha wagonjwa kubebwa kwa mitumbwi isiyo rasmi.

Nipashe ilifika eneo la tukio na kushuhudia wananchi wakihangaika kupita huku mitumbwi isiyo rasmi wagonjwa pamoja na wajawazito ili wakapate huduma upande wa pili huku nauli za mabasi zikipanda.

Mkazi wa Kata hiyo, Benjamin Daniel, alisema tangu mvua hizo zianze kunyesha eneo hilo limekuwa halipitiki hali iliyosababisha mmoja wa wajawazito kukosa usafiri na kujifungulia upande wa pili. Aidha, aliiomba serika kufanya juhudi za makusudi ikiwamo kuinua barabara hiyo kwa kifusi na kuweka madaraja imara yatakayosaidia maji kufuata mkondo wake na kuondoa adha ya barabara kukatika.

Mkazi mwingine wa wilaya hiyo, Mohamed Momange, alisema kwa sasa nauli ya kutoka Kaliua kwenda Uyungu zimepanda hadi Sh.12,000 kutoka nauli ya Sh.7,000 ambapo bado kuna malipo ya kuvushwa na mtumbwi ambayo ni kati ya Sh.2,000.

Mmoja wa wasafirishaji, Hamis Said, alisema nauli zimepanda kutokana na wao kulazimika kubadilishana wateja wa pande mbili kutokana na magari kushindwa kufuka katika eneo hilo.

"Magari yakifika upande ule tunabadilisha wanaletwa huku kwa mitumbwi au kwa miguu na sisi tunawapokea na kuendelea na safari lakini tatizo hili limekuwapo kwa zaidi ya miaka minne sasa kila wakija wanarekebisha maeneo yasiyo na matatizo wanaacha kufanyia kazi eneo hili," alisema Said.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) mkoani Tabora, Mhandisi Raphael Mlimaji, alifika katika eneo hilo na kuwataka wananchi kuwa wavumilivu wakati wakianza ukarabati wa eneo hilo.

"Awali zilitolewa fedha za dharura kwa ajili ya kilometa nne ambapo tulinyanyua tuta katika moja ya maeneo yaliyokuwa na shida mwaka jana lakini tutaanza pia huku ambapo tatizo limehamia," alisema Mhandisi Mlimaji.

# Mifumo chanzo ucheleweshwaji haki mahakamani

**Na Waandishi Wetu**

KUTOSOMANA kwa mifumo katika sekta ya haki jinai kumeelezwa kuwa miongoni mwa mambo yanayochelewesha utolewaji wa haki mahakamani ikifuatiwa vitendo vya rushwa kwa baadhi ya watumishi.

Hayo yameibuliwa kwa nyakati tofauti katika maadhimisho ya kilele cha siku ya sheria yaliyofanyika katika maeneo mbalimbali nchini mwishoni mwa wiki na kitaifa yakifanyika jijini Dodoma.

Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Tarime, Veronica Selemani, licha ya mnyororo wa haki jinai kukabiliwa na rushwa vinavyoendekezwa na baadhi ya watumishi wasiyokuwa waadilifu pia mifumo kutokusomana limekuwa tatizo linalochelewesha utoaji haki.

Aliomba kuboreshwa kwa mifumo hiyo ili isomane katika taasisi husika ikiwamo upelelezi wa makosa ya jinai, TAKUKURU, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Kitengo cha Kudhibiti na Kupambana na dawa za kulevya ili kurahisisha kazi hiyo inayosaidia mahakama kutekeleza wajibu wake.

"Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ifanye jitihada za kuandaa miswaada yenye kuakisi mabadiliko ya sheria yenye lengo la kuondoa vikwazo vya upatikanaji haki jumuishi, Bunge lifanyie marekebisho ya sheria zinazozuia upatikanaji wa haki jumuishi pale miswaada ya mabadiliko inapofika bungeni" alisema Veronica.

Wakili wa serikali, Tawabu Issa, alisema Ibara ya 107A(1) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inataja Mamlaka ya mwisho ya utoaji haki kuwa chini ya Mahakama ya Tanzania ingawa pekee haiwezi kufanikisha jukumu hilo.

Naye Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Sengerema, Tumsifu Barnabas, aliwaomba wananchi kuwa na mazoea ya kutembelea Mahakama ili kupata elimu ya TEHAMA na kuitumia pindi wapatapo kesi ili wasipate shinda ya kufungua kesi

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, aliwataka watumishi wa Mahakama kufata maadili ya kazi ili kuondokana na malalamiko ambayo huwa yanajitokeza kutoka kwa wananchi wanaokwenda kupata huduma.

Mwenyekiti wa Klabu ya Kupinga Rushwa, Shule ya Sekondari Nyampulukano, Moses Stesheni, aliziomba shule ambazo hazina klab hizo kuanzisha kwani zinasaidia kutoa elimu kwa wanafunzi ambao hawajui sheria.

**- Imeandaliwa na Elizabeth Seleman (SENGEREMA), Timoth Itembe (TARIME)**

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI SITA WA AFCON WANAOWEZA KUULA ULAYA UK. 12



# BOUCHRA KARBOUBI: MWAMUZI AFCON, POLISI NA MAMA

Bouchra Karboubi, akiwa kazini mechi ya Afcon kati ya Nigeria na Guinea-Bissau.

**ABIDJAN, Ivory Coast**

MWAMUZI wa Morocco, Bouchra Karboubi, ndiye aliyesimamia mechi ya Kundi A kati ya Nigeria na Guinea-Bissau kwenye Afcon kama sehemu ya timu ya waamuzi ya wanawake wote.

Bouchra ni msimamizi wa sheria. Akiwa uwanjani anatumia filimbi na kadi zake kuimarisha utulivu, lakini katika kazi yake ya kila siku, pingu ndio anayoitumia.

Ni mwamuzi wa kimataifa wa mpira wa miguu na polisi mwanamke huko Meknes, Jiji la Kaskazini mwa Morocco.

"Kuwa polisi mwanamke kwangu, kunamaanisha kutumia haki," anasema katika mahojiano na BBC Sport Africa.

"Kama mwamuzi, mimi hutumia sheria na ni kazi yangu ninayoipenda na zote mbili zina uhusiano."

Mnamo 2022, Salima Mukansanga wa Rwanda aliandika historia kwa kuwa mwanamke wa kwanza kuwa mwamuzi wa mechi ya Afcon ya wanaume nchini Cameroon.

Karboubi aliiga hilo mwezi uliopita, na aliongoza timu ya maofisa wa timu ya wanawake - mchuano mwingine wa kwanza - wakati Nigeria ilipoishinda Guinea-Bissau katika hatua ya makundi.

Jukumu kuu alilonalo Mmorocco huyu katika michuano inayoendelea linamfanya kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Afrika Kaskazini kuwa mwamuzi kwenye Afcon ya wanaume.

"Hisia zilikuwa kubwa sana. Ni heshima kwangu, kwa familia yangu, kwa nchi yangu na kwa wanawake wa Kiafrika kwa ujumla," anasema kuhusu ushiriki wake.

Mwanamke huyo mwenye umri wa miaka 36, hata hivyo, anaongeza kuwa kuna zaidi ya utambulisho wake zaidi ya kazi zake mbili.

"Ni kweli kazini mimi ni askari polisi na uwanjani ni mwamuzi, lakini nyumbani mimi ni mwanamke, mimi ni mama wa nyumbani na mama wa binti."

**Kuvunja mila potofu**

Katika ukuaji wake, Karboubi alipenda kucheza soka, lakini aliacha kwa sababu hakukuwa na soka la wanawake lililopangwa wakati huo. Kwa hivyo, aliamua kuingia kwenye mechi ambapo aliona fursa nyingi zaidi kama mwamuzi.

Karboubi alikabiliwa na upinzani kutoka kwa familia yake katika kufuata ndoto zake, akiwaambia Wanawake wa Muungano wa Mataifa ya Kiarabu mwaka 2021: "Ninatoka katika mji mdogo wa kihafidhina; kwa hiyo, ilikuwa ngumu kwa familia yangu kukubali ukweli kwamba nilitaka kuendeleza taaluma yangu ya michezo."

**Ndugu zake ndio walikuwa kikwazo chake kikubwa**

Waliwahi kupata bendera ya msaidizi wake na kuipasua na kumwacha Karboubi akilia, lakini aliishona na kuendelea na mazoezi.

Lakini mwaka wa 2007, baba yake alimtizama akiwa mwamuzi wa mchezo wa wanawake, na kuanzia hapo alipata usaidizi wa kufuata njia aliyochagua. Leo, yeye ni mwamuzi wa kwanza mwanamke wa Kiarabu uwanjani.

Kando na kuwa mwanamke wa kwanza Mwarabu kuwa mwamuzi wa mechi ya wanaume mnamo 2020, Karboubi pia ndiye mwanamke wa kwanza Mwafrika kufuzu kama mwamuzi msaidizi wa video (VAR).

Morocco na Misri ndizo nchi pekee barani Afrika ambazo zimetekeleza kikamilifu matumizi ya VAR katika ligi zao za ndani.

"Nina bahati kuwa Morocco kwa sababu ilikuwa nchi ya kwanza ya Kiafrika kuanzisha matumizi ya VAR," Karboubi anaelezea kuhusu jinsi alivyoanza kazi ya usimamizi wa video.

"Niliweza kuhudumu kama mwamuzi msaidizi wa video katika fainali za Afcon za 2021 kwa wanaume na ilikuwa heshima kwangu.

"Ilimaanisha kuwa wanawake wangeweza kufanya kazi katika maeneo yote kama wanaume. Daima tumepigana kuwa na wanaume. Tuliweza kuonyesha kwamba tunaweza kuwa huko."

Jukumu la kwanza la kimataifa alilotekeleza Karboubi kama mwamuzi lilikuwa ni Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake 2018 nchini Ghana.

**Inspekta wa polisi**

Bouchra alikuwa katika nafasi ya nne rasmi wakati wenyeji wa Afcon, Ivory Coast walipokutana na mabingwa watetezi Senegal katika hatua ya 16 bora.

Waamuzi wa kike kote ulimwenguni wanafanya vema kwenye mchezo huo mzuri. Mnamo 2022, Stephane Frappart wa Ufaransa alikua mwanamke wa kwanza kuchezesha Kombe la Dunia la Fifa kwa wanaume, akisimamia mchezo wa hatua ya makundi kati ya Costa Rica na Ujerumani.

Licha ya hatua hizi zilizopigwa hadi sasa, Karboubi anahisi wanawake bado lazima wapige hatua ya ziada ili kuthibitisha umahiri wao.

"Ni kweli wanawake ili kufikia kiwango hiki lazima wafanye kazi ya ziada, kwanza kimwili, kwa sababu ili kuwa tayari kwa mechi ya wanaume lazima tuwe sawa sawa na wanaume," anafafanua.

"Baada ya hapo utaalamu wa kiufundi, ambao lazima tuwe nao bila shaka, juu ya sheria za mchezo.

"Mwanaume akikosea watasema yeye ni mwanaume, ni binadamu tu. Lakini mwanamke atakosolewa mara mbili zaidi kwa sababu ni mwamuzi wa kike."

Akiwa kazini huko Morocco kipolisi, Karboubi ni Inspekta na hupata usaidizi kutoka kwa wafanyakazi wenzake ambao daima wana hamu ya kujua kuhusu majukumu yake ya uongozaji wake wa kazi.

"Wananiambia maneno kama; 'kwa nini haukufanya hivyo? Kwa nini ulifanya hivyo? Kwa nini ulipiga filimbi kwa penalti? Tueleze kwa nini kadi nyekundu' lakini daima wananitia moyo, na ninashukuru msaada wao," Karboubi alisema.

**Anaamini kazi hizo mbili zinafanana**

"Usimamizi ulinisaidia sana kama mwanariadha kuwa afisa mzuri wa polisi, na kuwa afisa wa polisi kulinisaidia kuwa mkakamavu uwanjani kama mwamuzi."

Akiwa ni mama wa mtoto mmoja ana matamanio ya kuchezesha Kombe la Dunia la wanaume siku moja, baada ya kusimamia kwa mara ya kwanza Fifa katika mashindano ya wanawake mwaka jana.


Anatumani kuwa mafanikio yake hadi sasa katika nyanja mbili zinazotawaliwa na wanaume yanaweza kuwatia moyo wanawake vijana katika ulimwengu wa Kiarabu.

"Inawezekana ilikuwa ni fani iliyotawaliwa na wanaume, lakini leo tumeweza kuonyesha kwamba hata wanawake wanaweza kufanya hivyo," alisema.

"Kwa hiyo, ningewaambia wasichana ambao wana lengo hilo kufanya kazi kwa bidii na kamwe wasikate tamaa."

## ISIKUPITE

AKIWA tayari anashikilia rekodi ya kufikisha mabao 20 katika mechi chache zaidi (14) za Bundesliga, bao alilofunga juzi wakati Bayern Munich ikishinda 3-1 dhidi ya Borussia Monchengladbach, linamfanya Harry Kane sasa kufikia rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi (24) baada ya mechi 20 za msimu wa Bundesliga, iliyowekwa na washambuliaji wawili wa zamani wa Bayern - Gerd Muller mnamo 1969-70 na Robert Lewandowski 2020-21.



## Extra Time

# WACHEZAJI SITA WA AFCON WANAOWEZA KUULA ULAYA


LAMINE CAMARA 2

**ABIDJAN, Ivory Coast**

KLABU za Ulaya zinafuatilia kwa karibu wachezaji waliofanya vizuri kwenye mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), ambao wameonesha kiwango kizuri na cha kuvutia.

Wakati michuano hiyo ikielekea hatua ya nusu fainali, makala haya yanawaangalia nyota sita ambao huenda wakanyakuliwa na klabu kubwa Ulaya.

Wanne kati yao bado hawajacheza katika ligi yoyote kati ya ligi tano bora za Ulaya. Na watatu wakiwa wenye umri wa miaka 22 au chini ya hapo.

Dirisha dogo la uhamisho la wachezaji lilifungwa Alhamisi, huenda muda si mrefu wanunuzi wataanza kuwasilisha ofa zao kwa ajili ya dirisha la majira ya joto...

**#1. Lamine Camara - Senegal**

Lamine Camara kutoka Klabu ya Metz ya Ufaransa na Taifa la Senegal, ni kiungo wa kati. Ametajwa kuwa Mwanasoka Bora Chipukizi wa Bara la Afrika Desemba 2023.

Camara mwenye umri wa miaka 20, alijitangaza kwa kufunga mabao mawili na kuwa mchezaji bora wa mechi katika ushindi wa Senegal wa 3-0 dhidi ya Gambia.

Haikuwa mara ya kwanza kwa Camara kufunga mabao mawili katika mchezo mmoja kwenye mashindano ya kimataifa.

Alifunga mabao mawili wakati Senegal ilipoishinda Tunisia katika Afcon ya vijana chini ya umri wa miaka 20 mwaka 2023, huku pia akiwa kwenye kikosi cha wakubwa kilichotwaa ubingwa wa Mataifa ya Afrika mwaka jana.

Kiungo wa kati ambaye ni zao la akademi ya Senegal ya Generation Foot, ambayo imezalisha wengine kama Sadio Mane - alifanikiwa kwa asilimia 84 ya pasi zake kabla ya 'Simba wa Teranga' kutupwa nje ya michuano hiyo na Ivory Coast hatua ya 16 bora.

Camara alijiunga na Metz, Februari mwaka jana na kujitengenezea jina Oktoba akifunga bao dhidi ya Monaco kwenye mechi ya Ligue 1.

**#2. Jesus Owono - Equatorial Guinea**

Owono ni kipa wa Alaves ya Hispania na Equatorial Guinea, alishinda tuzo ya mchezaji bora wa mechi katika sare ya kwanza ya Equatorial Guinea dhidi ya Nigeria na katika mechi ya ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Ivory Coast.

Owono alicheza bila kufungwa katika mechi tatu katika mechi nne za Kombe la Mataifa ya Afrika 2021 na kuokoa penalti mbili katika ushindi wa mikwaju ya penalti dhidi ya Mali na timu yake ikatinga robo fainali.

Owono anaweza kuwa mlinda mlango mkubwa barani Afrika - akifuata nyayo za magwiji kama Carlos Kameni wa Cameroon na Thomas N'Kono na Vincent Enyeama wa Nigeria.

**#3. Emmam Ashour - Misri**

Ashour ni mchezaji wa Al Ahly na Misri, alikuwa bora katika kutoa usaidizi wa ulinzi na kusonga mbele ili kuongeza mashambulizi ya Misri wakati wa mechi zao za Kundi B.

Licha ya kucheza kwa dakika chache zaidi ya wachezaji wenzake wengi, Ashour bado alimaliza akiwa kileleni kwa kutengeneza nafasi, pasi, kutamba na mpira, kukabiliana na adui - akiwa chini ya mchezaji Mostafa Mohamed.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alicheza kwa muda mfupi na mabingwa mara tatu wa Denmark, Midtjylland mwaka 2023, akifunga kwenye mechi yake ya kwanza ya Europa League na Superliga na kisha kuhama kwenda Zamalek ya Misri kwa ada ya pauni milioni 2.6.

Alirejea katika Ligi Kuu ya nchi yake akiwa na Al Ahly Julai mwaka jana. Je, ataweza kurudi tena katika klabu yoyote ya Ulaya?

**#4.Aboubakary Koita - Mauritania**

Koita anayecheza Sint-Truiden ya Ubelgiji na Taifa la Mauritania alizitimiza ndoto za taifa lake kusonga mbele.

Mchezaji mwenye kasi, kinda huyo mwenye umri wa miaka 25, winga mwenye jicho la kulenga lango - aliisaidia timu yake kutinga hatua ya 16 bora, na kujihakikishia ushindi wa kwanza kabisa kwenye michuano hiyo walipowalaza mabingwa wa Afcon 2019, Algeria kwa bao 1-0.

Bao la Koita ambalo moja ya mabao ya masafa marefu katika mechi waliyofungwa 3-2 na Angola wakati wa hatua ya makundi, litakuwa miongoni mwa mabao bora ya michuano hiyo.

Mzaliwa wa Senegal, Koita ni mchezaji wa Sint-Truiden ya Ubelgiji - nchi ambayo aliishi maisha yake ya ujana, baadaye alitumia miaka miwili akichezea kwa mabingwa wa zamani, Gent.

**#5. Gelson Dala - Angola**

Gelson Dala amefunga kila baada ya dakika 79 kwa wastani kwenye fainali za Afcon 2023 kabla ya mechi ya robo fainali ya Angola dhidi ya Nigeria.

Dala ni mchezaji wa Klabu ya Al Wakrah ya Qatar. Ameshinda mara nne na kuisaidia Angola kufuzu robo fainali kwa mara ya kwanza tangu 2010, na hivyo kumfanya kuwa nyuma kwa bao moja dhidi ya kinara Emilio Nsue.

Baada ya mabao mawili dhidi ya Mauritania katika hatua ya makundi, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alifunga mabao mengine mawili na kuweka bao katika ushindi wa 3-0 dhidi ya Namibia katika hatua ya 16 bora.

Ufungaji wa Dala akiwa Angola akiwa kijana ulisababisha miamba ya Ureno, Sporting CP kumsajili mwaka 2017, lakini hakuweza kuingia kwenye kikosi chao cha kwanza na alikaa kwa msimu mmoja huko Rio Ave mnamo 2020-21.

Tangu ajiunge na Klabu ya Al Wakrah ya Qatar mwaka 2022 amekuwa na wastani wa kufunga wa zaidi ya goli katika kila mchezo.

**#6. Aguibou Camara - Guinea**

Umaliziaji wa Camara uliipa Guinea ushindi muhimu dhidi ya Gambia, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amefanya kazi kubwa katika kila dakika ya mbio zao za robo fainali.

Mchezaji wa Atromitos ya Ugiriki, amepata uzoefu katika Ligi ya Mabingwa na Ligi ya Ulaya tangu ajiunge na Olympiacos mwaka 2021 na kwa sasa yuko kwa mkopo katika timu ya Atromitos ya Ligi Kuu ya Ugiriki.

Mshambulizi huyo mahiri, ambaye pia anaweza kucheza katika safu ya kiungo, tayari ameshawekwa katika nafasi mbalimbali na Guinea wakati wa mechi zao, na alizungumzia utayari wake wa kubadili namba baada ya kuombwa na meneja Kaba Diawara wakati wa mechi za makundi.

## Nukuu

"Binafsi, Messi labda ndiye pekee. Nilipenda kumwangalia mchezaji [wa zamani] wa Barcelona, chini ya hapo mwishoni, lakini ndiye mkubwa zaidi katika historia. Haiwezekani kumpokonya mpira. Cristiano ni mchezaji mkubwa kuliko mimi lakini, katika historia, kwa upande wa soka halisi, kiukweli sifikirii hivyo. Neymar, labda," **Eden Hazard anaamini kuwa alikuwa na kipaji kikubwa zaidi ya Cristiano Ronaldo huku akidai Lionel Messi pekee ndiye anayemzidi.**



"Hakufunga lakini amekuwa na mchezo mzuri sana. Si rahisi kumzuia mtu huyo. anatengeneza nafasi. Ni mzuri kwa timu yetu," **Kocha wa Nigeria, Mreno Jose Peseiro, akimzungumzia mshambuliaji Victor Osimhen, ambaye hadi sasa ana bao moja tu kwenye michuano ya Afcon inayoendea nchini Ivory Coast.**



"Huu si wakati wa kuongea kuhusu kocha, Xavi ametushangaza. Tulikuwa tunamtegemea Xavi mwakani," **Mkurugenzi wa Michezo wa Barcelona, Deco, baada ya Xavi kutangaza ataachia ngazi mwishoni mwa msimu.**






Kiungo Mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza, akikimbia kwenda kushangilia bao pekee alilofunga kwa mkwaju wa penalti katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Uwanja wa Lake Tanganyika, mjini Kigoma juzi. Nyuma yake ni Sadio Kanoute akimfuata kumpongeza, pembeni ni kiungo wa Mashujaa FC, Balama Mapinduzi, akionyesha kusikitika. **MPIGAPICHA WETU**

# REKODI 5 LIGI KUU BARA IKIREJEA KWA KISHINDO

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Ligi Kuu Tanzania Bara imerejea baada ya siku 39 za mapumziko kupisha, kwanza Kombe la Mapinduzi lililofanyika mjini Zanzibar na Mlandege kuwa mabingwa na pili kupisha Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), ambapo Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars ilikuwa ikishiriki.

Mechi mbili zilizochezwa Ijumaa na Jumamosi ziliashiria kurejea tena kwa kinyang'anyiro hicho cha kumsaka bingwa wa Tanzania Bara.

Febrauri 2, Mabingwa Watetezi Yanga, walikuwa kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera kucheza dhidi ya wenyeji, Kagera Sugar na kesho yake, Mashujaa FC waliikaribisha Simba kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma.

Michezo hiyo miwili imetengeneza rekodi kadhaa ambazo zinaainishwa katika makala haya.

**1. Yanga kupata sare ya kwanza**

Dakika 90 za mchezo kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera zilimalizika Ijumaa iliyopita, Yanga ikiweka rekodi ya kupata sare ya kwanza tangu kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara, Agosti 15, mwaka jana.

Ilitoka bila kufungana na Kagera Sugar na kabla ya hapo haikuwa na sare hata moja, badala yake ilikuwa imecheza mechi 11, ikishinda 10 na kupoteza moja ilipofungwa mabao 2-1 dhidi ya Ihefu FC, Oktoba 4, mwaka jana.

**3. Simba kushinda mechi zote mikoani**

Ushindi wa bao 1-0 ilioupata Simba kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma, umeifanya timu hiyo kushinda mechi zote ilizocheza kwenye viwanja vya mikoani, ikiwa na asilimia 100 ya ushindi.

Imecheza mechi nne kwenye viwanja vya ugenini, ambapo ilianza kwa ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Mtibwa Sugar, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro, ikaenda kwenye Uwanja wa Liti, Singida, ikaiadhibu Singida Fountaine Gate mabao 2-1, kabla ya Jumamosi iliyopita kufanya tena hivyo mjini Kigoma.

**2. Yanga kutofunga bao dakika 90**

Katika mechi ya Ijumaa dhidi ya Kagera Sugar, timu ya Yanga imeshindwa kufunga bao lolote kwa dakika 90 za mchezo kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Katika mechi 11 ilizocheza, ilikuwa ikipata bao angalau moja kila mchezo, lakini rekodi hiyo imekuja kutibuliwa na Kagera Sugar baada ya kuing'ang'ania suluhu.

Mechi 11 ilizocheza ilipata ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya JKT Tanzania na KMC, ikaichapa Simba mabao 5-1, ikashinda bao 1-0 dhidi ya Coastal Union, Namungo FC na Tabora United, mabao 3-2 dhidi ya Azam FC, 3-0 dhidi ya Geita Gold, ikashinda mabao 4-1 dhidi ya Mtibwa Sugar, mabao 2-0 dhidi ya Singida Fountain Gate.

Hata ilipopoteza mechi dhidi ya Ihefu, ilipata bao moja, ikifungwa mabao 2-1.

**4. Simba wakali wa penalti, Saido akiongoza**

Linakuwa ni bao la tano kwa Saido Ntibazonkiza, manne akiyafunga kwa mkwaju wa penalti, lingine akifunga katika mechi dhidi ya KMC ilipotoka sare ya mabao 2-2, Kagera Sugar, iliposhinda mabao 3-0 na Prisons iliposhinda 3-1.

Pia linakuwa ni bao la tano kwa Simba kufunga kwa penalti ikiwa ndiyo timu inayoongoza kwenye Ligi Kuu kwa kupata penalti nyingi mpaka sasa na zote imezikwamisha wavuni.

Penalti pekee ambayo haikupigwa na Saido, ni dhidi ya Coastal Union, Simba ikishinda mabao 3-0, yenyewe iliwekwa wavuni na Jean Baleke ambaye kwa sasa hayupo kwenye kikosi cha timu hiyo.

**5. Simba haijapoteza Lake Tanganyika**

Kwa miaka minne, Simba haijapoteza mechi yoyote kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika jijini Kigoma.

Ni kama ina nyota nzuri na uwanja huo, kwani wakati juzi ikiichapa Mashujaa FC bao 1-0, mara ya mwisho kuondoka hapo ilikuwa Julai 25, 2021 ilipotoa kipigo cha bao 1-0 dhidi ya mahasimu wao wa jadi, Yanga katika fainali ya Kombe la FA.

**JE, WAJUA?**



WAKATI ambao labda utakumbukwa zaidi kwenye Fainali za Afcon 2023 nchini Ivory Coast ni katika mechi ya robo fainali kati ya Cape Verde na Afrika Kusini, ambapo uokoaji wa hali ya juu ulionekana pale kipa na nahodha wa Afrika Kusini, Ronwen Williams, alipoipeleka nusu fainali timu yake kwa kuokoa penalti nne. Haitashangaza akitwaa tuzo ya kipa bora wa michuano hiyo.



# Bil. 6.9/ kuboresha utoaji elimu kupitia TEHAMA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Awali na Msingi (BOOST) imetoa vifaa vya TEHAMA vyenye thamani ya Sh. bilioni 6.9 kuwezesha wanafunzi wasio na walimu wa masomo husika kufundishwa kwa njia ya mtandao na walimu waliopo shule zingine ili kuimarisha utoaji wa elimu nchini.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa ugawaji wa vifaa hivyo kwa vituo vya walimu wa awali na msingi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, imenunua vifaa hivyo kutekeleza azma ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuboresha mazingira ya upatikanaji wa elimu nchini.

Alisema pia imetoa mafunzo kwa walimu wa TEHAMA takribani 400 wa shule za msingi na sekondari ili utekelezwaji wa programu hizo ufanyike kwa umahili.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo anayeshughulikia Elimu, Dk.Charles Msonde, alisema vifaa hivyo vitatumika kuboresha mafunzo ya walimu endelevu katika maeneo yao na kufundisha wanafunzi.

"Kupitia teknolojia walimu watakuwa na uwezo wa kufundishwa na wataalamu na kubadilishana mawazo wakiwa kwenye vituo vyao vya kazi kupitia vifaa vya TEHAMA.

Kutakuwa na kazi nyingine ya kuwawezesha wanafunzi kusoma katika teknolojia ya sasa hivi na upo uwezekano wa mwalimu bora wa Fizikia kufundisha wanafunzi wengi katika shule mbalimbali kwa hiyo vifaa hivi," alisema.

Alisema tayari majaribio ya kutumia njia hiyo ya kufundisha kwa mtandao yamefanyika hivi karibuni katika shule za sekondari Kibaha na Dodoma.

"Tumeshafanya majaribio hivi karibuni tulifunga vifaa vya TEHAMA Kibaha, itakuwa kituo maalum cha teknolojia ya TEHAMA ambapo mwalimu mzuri wa Kibaha atafundisha shule zisizo na walimu na wanafunzi watasikiliza na kuuliza maswali, ni malengo ya serikali ya awamu ya sita ya kuboresha elimu na walimu wamekuwa wakifanya kazi kubwa," alisema.

Aidha, alisema katika hafla hiyo yamegaiwa magari 13 ambayo yamenunuliwa kupitia mradi wa KKK(GPE-LANES) kwa ajili ya Maofisa Elimu wa Elimu ya awali na msingi ,na ni mwendelezo wa uboreshaji sekta ya elimu.

Alisema tangu mwaka 2021 serikali imeshatoa Sh.bilioni 40.3 kwa ajili ya kununua magari 432 ambayo yamegaiwa kwa maofisa elimu msingi na sekondari kwenye halmashauri na mikoa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Denis Londo, alipongeza kazi kubwa iliyofanywa na serikali inayoongozwa na Rais Samia ya kuimarisha mazingira ya utoaji elimu.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema uandikishwaji wa wanafunzi katika Mkoa wa Dodoma, mpaka juzi umefikia asilimia 92 kwa upande wa elimu ya awali, asilimia 95 kwa darasa la kwanza na asilimia 67.

Pia aliahidi kwa niaba ya wakuu wa mikoa wengine kuhakikisha wanasimamia utunzaji wa magari na vifaa vya TEHAMA ambavyo vimeelekezwa katika maeneo yao.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU), Vita Kawawa (kulia), akiagana na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, baada ya semina iliyoandaliwa na Jeshi la Magereza kwa ajili ya kamati hiyo, iliyohusu utendaji kazi wa jeshi jijini Dodoma jana. Katikati ni Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Miriam Mmbaga. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

# Wenyeviti mitaa wanyooshewa kidole uuzaji holela wa viwanja

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKURUGENZI wa Jiji la Dodoma, John Kayombo, amesema kuwa baadhi ya wenyeviti wa serikali za mitaa wamekuwa wakijihusisha na uuzaji wa viwanja kwenye maeneo yaliyopimwa na yasiyopimwa na kusababisha kuwapo kwa migogoro na chuki kati yao na wananchi.

Kayombo aliyasema hayo alipokuwa akitoa taarifa kwa kamati ya siasa ya Mkoa wa Dodoma ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), baada ya kuhitimisha ziara ya kukagua ujenzi wa majengo ya shule ya sekondari ya Michese na barabara zinazojengwa jijini humo.

Alisema moja ya kero kubwa iliyopo kwenye halmashauri hiyo ni kwa baadhi ya wenyeviti kujihusisha kuuza viwanja kwenye maeneo yao na kusababisha watendaji wa Jiji hilo kufanya kazi kwenye mazingira hatarishi.

Alieleza kuwa pamoja na mafanikio yaliyopo yakiwamo ya kugawa viwanja na kulipa fidia kwa wale wanaostahili kwa waliopitiwa miundombinu mbalimbali, kuna kila sababu ya CCM kutoa karipio kali kwa wanaojihusisha na tabia hiyo.

"Pamoja na sisi baadhi ya watumishi wetu wa halmashauri kuwa na upungufu tumekuwa tukinyooshewa vidole na wananchi na wakati mwingine kupigwa, kujeruhiwa na kuharibiwa vitendea kazi pale wanapowataka waondoke maeneo hayo waliyoyavamia na huku wengine wakidai kuuziwa na viongozi wasio na uaminifu kwenye nafasi zao," alisisitiza.

Aliwasihi viongozi wa juu wa chama hicho wasiwapitishe kugombea nafasi ya uenyekiti wa mitaa viongozi wanaowagombanisha watumishi wa Jiji na wananchi wanaovamia maeneo ya ardhi yaliyopimwa na yale yaliyotegwa kwa shuhuli za kiserikali na taasisi.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC), Donald Mejetii, alishauri Jiji hilo kuimarisha ulinzi kwenye maeneo yao ili yasivamiwe na kuepukana na migogoro ya mara kwa mara kati yao na wananchi.

"Ni kweli kuna baadhi ya watumishi wa chama na serikali wakiwamo wenyeviti wa serikali za mitaa, wamekuwa wakisababisha migogoro kwenye maeneo yao na wengine wakiwachochea wananchi kuandamana, kuzuia tena wakiwa wameshika silaha pale wanapotakiwa kuondoka,"alisema.

# ARMP yatua nchini kupata uzoefu wa usimamizi ununuzi wa umma

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAOFISA wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma Burundi (ARMP) wapo nchini kupata uzoefu wa serikali ya Tanzania katika kuboresha ufanisi katika usimamizi wa ununuzi wa umma.

Maofisa hao watajifunza pia maendeleo ya Mfumo wa Kitaifa wa Ununuzi wa Kielektroniki Tanzania (NeST) wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma Tanzania (PPRA).

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Mtendaji Mkuu wa PPRA, Eliakim Maswi, alisema kuwa ziara ya Mamlaka ya Burundi ni sehemu ya ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki katika kubadilishana maarifa.

Alitaja kipengele kimojawapo kilichoivutia serikali ya Burundi ni mpango wa Tanzania katika kujenga Mfumo wa NeST unaoongeza uwazi, uwajibikaji na ushindani wa haki ili kuhakikisha thamani ya fedha inatumika katika mchakato wa manunuzi ya umma.

"Tunashirikiana katika maeneo mengi na kujifunza kutoka kwa kila mmoja, tunapokwenda Burundi tunajifunza kutoka kwao, wakija Tanzania wanajifunza hatua tunazochukua kuboresha usimamizi wa manunuzi ya umma, na hii ni sehemu ya maazimio ya ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema Maswi.

"Desemba mwaka jana, tulikuwa mwenyeji wa ujumbe kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), ambao unasimamia miradi mikubwa ya kilimo nchini Tanzania, Burundi na nchi nyingine," alisema na kuongeza.

Aliongeza "Tulipowasilisha kuhusu jinsi Mfumo wa NeST unavyofanya kazi, waliona ni hatua muhimu na chanya, na IFAD inashirikiana nasisi ili kuhakikisha mafanikio na matumizi yake."

Aidha, aliitaja PPRA kuwa imeonyesha baadhi ya miradi mikubwa inayofanywa na Serikali ya Tanzania mjini Dodoma kupitia taratibu za manunuzi ya umma, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Mji wa Serikali wa Mtumba, unaojulikana pia kama Magufuli City.

Aidha, alisema viongozi hao wa Burundi wamejulishwa kuhusu Sheria mpya ya manunuzi ya umma iliyotiwa saini na Rais Samia Suluhu Hassan, mwaka jana ili kujifunza kuhusu maboresho yaliyofanywa ili waweze kupata uzoefu muhimu.

Maswi alisisitiza umuhimu wa hatua hiyo kwa kuzingatia kwamba nchi za Afrika Mashariki ziko katika mchakato wa kukubaliana juu ya sheria ya umoja ya manunuzi ya umma.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa ARMP-Burundi, Nduwimana Cloude, alieleza kufurahishwa kwao na mpango wa Tanzania wa kujenga Mfumo wa NeST kwa kutumia wataalamu wa ndani.



# Daraja lakosesha wanafunzi elimu Rungwe

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WATOTO wa Kijiji cha Nzunda, Kata ya Ndato wilayani Rungwe, Mkoa wa Mbeya wanashindwa kuhudhuria shuleni kutokana na kukosekana kwa daraja kwenye korongo linalotenganisha kitongoji hicho na mahali ilipo shule.

Kutokana na hali hiyo, wakazi wa kitongoji hicho wameiomba serikali pamoja na wadau kuwasaidia kujenga daraja kwenye korongo hilo ili kutatua kero hiyo ambayo inawaathiri zaidi kipindi hiki cha mvua.

Walitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Maofisa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) waliotembelea kitongoji hicho kwa ajili ya kukagua miradi mbalimbali ya wanufaika wa mfuko huo ikiwamo katika sekta ya elimu.

Mmoja wa wananchi hao, Oliver Anyela, alisema korongo hilo limekuwa likipanuka mwaka hadi mwaka na limekuwa kubwa hata watu wazima wanapata shida kuvuka kwenda ng'ambo ya pili.

Alisema hali hiyo inawapa wasiwasi kwamba kama ikiendelea huenda kijiji chao kikakosa wasomi siku za usoni kutokana na korongo hilo kuathiri ratiba za masomo kwa watoto wao hao.

"Hapa mmesema kuna watu wa Benki ya Dunia na sisi tunatamani watoto wetu wasome waje wafanye kazi huko kwa hiyo tunaomba mtusaidie kujenga daraja kwenye korongo hili maana ni kubwa sana na watoto wanashindwa kuvuka," alisema Oliver.

Mmoja wa wanakijiji, Neema Sanga, alisema wanashindwa kujenga daraja la miti kutokana na korongo hilo kuwa kubwa na kuongezeka kila mwaka hali ambayo inahatarisha maisha yao. Alisema wakati mwingine huwa wanalazimika kuwasindikiza watoto wao shuleni na kwamba mvua ikinyesha hata wao wanashindwa kuvuka na kuwafikisha watoto shuleni na hivyo kuwafanya wasiende kabisa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nzunda, Pokea Mbilinyi, alisema korongo hilo mbali na kuathiri masomo kwa wanafunzi, pia linaathiri shughuli zingine za maendeleo kwa wananchi wake ikiwamo shughuli za kilimo na biashara.

Alisema wananchi wa kitongoji hicho wanazalisha mazao mbalimbali lakini kuyasafirisha kwenda sokoni inakuwa vigumu hasa kipindi cha masika kwa maelezo kuwa hakuna gari inayoweza kufika wala chombo chochote cha usafiri.

"Lakini hata barabara inayoelekea kwenye kitongoji hiki ina hali mbaya sana, tunaomba TARURA watusaidie kuiangalia ili kutatua kero hizi, mkitusaidia kukiunganisha kitongoji hiki mtakuwa mmetusaidia sana," alisema Mbilinyi.

Kaimu Mratibu wa TASAF Wilaya ya Rungwe, Robert Sewingwa, alisema mfuko huo huwa unafadhili miradi mbalimbali kwenye vijiji vyenye wanufaika ikiwamo miundombinu ya elimu, afya na barabara.

Alisema wananchi wa kijiji husika ndio wanachagua miradi ambayo wanataka itekelezwe kulingana na mahitaji yao na kwamba endapo fedha zitapatikana wananchi hao wataamua wenyewe kulingana na vipaumbele.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Elisha John, alisema kero zote za wananchi wa kijiji hicho wanazichukua na zitafanyiwa kazi kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana ili kuhakikisha huduma zinakuwa bora.

Alisema lengo la ziara hiyo ilikuwa ni kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili wakibaini matatizo waangalie namna ya kuyatatua ili wananchi wafanye shughuli zao za maendeleo bila vikwazo.



Mmoja wa wananchi wa Mkoa wa Mbeya akiwasilisha kero zake kwa viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa mkoa huo (hawapo pichani), mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa kusikiliza kero uliofanyika katika kituo cha daladala cha Kabwe, kushoto ni Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, John Nchimbi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wapanda parachichi kupambana na udumavu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SHULE ya Sekondari ya Wasichana ya Manyunyu iliyopo Lupembe wilayani Njombe katika Mkoa wa Njombe imepanda miche ya parachichi kwa lengo la kupambana na tatizo la udumavu na utapimlo kwa wanafunzi.

Matunda hayo yalipandwa mwishoni mwa wiki wakati wa mwendelezo wa maadhimisho ya miaka 47 ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambapo viongozi wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa chama hicho wilayani Njombe waliongoza upandaji miti huo.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Njombe, Sure Mwasanguti, alisema walichofanya UWT ni kuenzi kazi anazofanya Rais Samia Suluhu Hassan ya kupambana na udumavu na utapiamlo.

"Mmemuunga mkono Dk. Samia Suluhu Hassan na nyinyi mmepanda parachichi ambapo watoto wetu watakula chakula bora kwa lengo la kuondoa udumavu kwenye mkoa wetu wa Njombe hapa UWT mmeweka alama," alisema Mwasanguti.

Mwasanguti alisema kupandwa kwa miti hiyo shuleni hapo itasaidia watoto hao kupata matunda pamoja na kutunza mazingira.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi UWT Wilaya ya Njombe, Beatrice Malekela, alitoa wito wa wanachama kuendelea kushikamana wakati wakisherehekea miaka 47 ya chama hicho.

"Niwaombe sasa ndugu zangu tuendelee kushirikiana na kushikamana kwa pamoja na kuto kudanganyika na hiyo ndio dhamira ya Chama Cha Mapinduzi ili tuendelee kufika mbali," alisema Malekela.

Diwani wa Viti Maalumu Kata ya Lupembe, Faraja Mbaga, alipongeza uongozi wa CCM wilaya pamoja na Jumuiya kwa kufikiria kwenda kupanda miti kwa ajili ya matunda kwa ajili ya wanafunzi kwa lengo la kuendelea kutokomeza udumavu.

# Mkurugenzi apewa siku 14 kumaliza kero ya taka

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimetoa siku 14 kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji hilo, John Nchimbi kumaliza tatizo la takataka kuzagaa kwenye makazi ya watu ili kuepuka mlipuko wa magonjwa kikiwamo kipindupindu.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa chama hicho mkoa, Patrick Mwalunenge, kwenye mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua uliofanyika katika Kituo cha Daladala cha Kabwe jijini humo.

Alitoa agizo hilo kufuatia malalamiko ya wananchi wa jiji hilo ambao walidai kuwa kwa sasa takataka zinazagaa kwenye makazi yao bila kuzolewa kwa muda mrefu liche ya kuchangia fedha za uzoaji wa taka hizo kila mwezi.

Mmoja wa wananchi hao, Ebron Mwakibete Mkazi wa Soweto, alisema wamekuwa wakirundika taka kwenye maeneo yao wakitegemea kuwa zitaondoshwa na wazabuni walioingia mikataba na jiji lakini zinakaa muda mrefu bila kuondoshwa.

Alisema takataka hizo zikikaa kwa muda mrefu zinatoa harufu na hivyo kuwasababishia hofu ya kupata magonjwa ya mlipuko hasa kipindi hiki cha mvua.

Alisema awali walikuwa wanahifadhi taka hizo kwenye maghuba ambayo yalikuwa yamewekwa na jiji hilo kwenye maeneo yao lakini baada ya kuondoshwa maghuba hayo wanahifadhi kwenye makazi yao kama wanavyoelekezwa na viongozi.

"Kwa sasa tunaishi na uchafu kwenye nyumba zetu na baadhi ya wananchi wanazimwaga kwenye mito jambo ambalo ni hatari, tunaomba mtusaidie kutatua kero hizi," alisema Mwakibete.

Naye Chifu George Lyoto alisema hali ya jiji hilo ni mbaya na inahatarisha maisha ya wananchi na hivyo akawaomba viongozi wa CCM kuchukua hatua ili kuwanusuru wananchi na maradhi yanayoweza kutokea kwenye maeneo yao.

Akijibu kero hiyo, Mkurugenzi wa Jiji hilo, Nchimbi alisema kinachosababisha kero hiyo kuwa kubwa ni tabia ya wananchi wa jiji hilo kutokuwa na utamaduni wa kutunza mazingira na hivyo kutupa taka hivyo.

Alisema awali walikuwa wanatumia utaratibu wa kuweka maghuba kwenye maeneo mbalimbali lakini utaratibu huo haukufanikiwa kutokana na uendeshaji wake kuwa mgumu.

Alisema kwa sasa wameingia mkataba na Kampuni ya Suma JKT, kuzoa taka hizo katika Kata sita za Tarafa ya Sisimba na kwamba kampuni hiyo imeshaanza kazi na kwamba imeahindi kuongeza vifaa yakiwamo magari ambayo yameagizwa kutoka China.

"Tumewapatia hizo kata lakini kama ufanisi wao utakuwa mzuri tutawaongeza na kata zingine, lakini tunaendelea kuwaimarisha wazabuni wengine wadogo ili na wao wafanye kazi hii kwa ufanisi," alisema Nchimbi.

Baada ya maelezo hayo, Mwenyekiti wa CCM Mwalunenge alisema wana taarifa kuwa mzabuni mpya aliyeingia mkataba na jiji hilo ufanisi wake pia ni wa kusuasua kutokana na sababu ambazo hazieleweki.

"Sasa sisi kama chama tunatoa siku 14 kama ambavyo mlipewa na madiwani ili jiji hili liwe safi, hatutaki kuona eneo lolote kuna tatizo la uchafu tena," alisema Mwalunenge.

Alishauri Jiji hilo linunuwe magari yake ya kuzolea taka hizo na liwe linayakodisha kwa wazabuni ambao watapata tenda ya kuzoa taka hizo ndani ya jiji.





## Mariam Mwinyi asihi wazazi kuimarisha lishe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKE wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi, ameisisitiza jamii kuimarisha lishe kama njia ya kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano.

Mama Mariam ambaye ni Msarifu na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), aliyasema hayo katika mkutano wa kitaifa wa afya na lishe uliofanyika visiwanu humo juzi.

Alisema utafiti wa kitaifa uliofanyika Zanzibar kuhusu masuala ya lishe mwaka 2017, ulionesha kuwa asilimia 21 ya watoto chini ya miaka mitano walikuwa na udumavu na zaidi ya robo tatu walikuwa na upungufu wa damu.

Alisema kuwa asilimia 70 ya watoto hao walitokea katika mkoa wa Kaskazini Pemba na asilimia 68 walikua wa mkoa wa Kusini Pemba jambo ambalo linaathiri ukuaji wao katika kama vile kujifunza na mwili kupambana na magonjwa.

Aliongeza kuwa kupitia utafiti huo kiwango kikubwa cha utapiamlo kiliripotiwa kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa ambapo asilimia 43 waliripotiwa kuwa na tatizo hilo.

"Wanawake wajawazito wenye upungufu wa damu hukabiliwa na changamoto nyingi kama vile vifo vinavyotokana na uzazi, uvumilivu mdogo wa kutokwa na damu wakati wa kujifungua, kujifungua watoto wenye uzito mdogo na uwezo mdogo wa kupambana na maambukizi," alisema Mama Mariam. Alitaja baadhi ya sababu za utapiamlo nchini kuwa ni matunzo duni ya mama na mtoto, tabia za uchaguzi wa chakula na upishi usiofaa na ulishaji watoto wachanga usiozingatia lishe bora.

"Siku 1,000 za mwanzo wa maisha ya mtoto ni kipindi muhimu kwa ukuaji wa ubongo yaani hivyo kuimarisha lishe ya wanawake, upatikanaji wa huduma za lishe na ushauri wa lishe kabla na wakati wa ujauzito pia wakati wa kunyonyesha ni muhimu katika kuzuia utapiamlo," alisema. Aidha aliitaka Wizara ya Afya kuhakikisha, elimu ya afya na lishe inatolewa katika ngazi ya jamii kupitia wahudumu wa afya ngazi ya jamii ambao wanapatikana kila kaya. Aliipongeza Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa jitihada inazofanya ikiwamo ya kuzindua mwongozo wa taifa wa chakula na ulaji ili kuhamasisha matumizi sahihi ya chakula mchanganyiko kutokomeza changamoto za utapiamlo hapa nchini.

Alilishukuru Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kwa kufadhili wa mradi wa lishe uliotekelezwa kwa pamoja kati ya Taasisi ya Benjamin Mkapa Foundation na Zanzibar Maisha Bora Foundation katika wilaya za Kaskazini 'A' na Micheweni Pemba. Naye Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Khafidh, alisema kuwa wizara yake itaendelea kusimamia misingi bora ya uwajibikaji na kupongeza wadau na washirika wa maendeleo kwa kufadhili shughuli za mradi huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Benjamin Mkapa, Dk. Anna Senkoro, alisema kuwa katika utekelezaji wa mradi huo wamefanikiwa kuandaa mwongozo wa mafunzo na elimu ya lishe kupitia wahudumu wa afya ya jamii 90 katika shehia za Wilaya za Kaskazini 'A' na Micheweni Pemba.

# Wizara yaita wadau kutoa maoni marekebisho Sera Mambo ya Nje

**NA Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeandaa kongamano la ukusanyaji wa maoni kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya sera mpya ya mambo ya nje itakayoendana na mahitaji ya nchi.

Kongamano hilo litakalowakutanisha wadau mbalimbali ikiwamo wanasiasa, viongozi wa dini, asasi za kirai na wananchi litafanyika leo visiwani Zanzibar na kwa upande wa Pemba litafanyika Februari 10.

Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi, Adila Hilal Vuai, aliwaambia waandishi wa habari juzi kuwa sera inayotumika sasa imetayarishwa mwaka 2001 ambapo ni kipindi kirefu wakati sasa kuna mambo mengi yamejitokeza yanatakiwa kujumuishwa.

Alisema mchakato wa kufanya maboresho hayo ni uamuzi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan pamoja na Rais wa Zanzibar, Dk.Hussein Ali Mwinyi wa kutaka kuwepo kwa ushiriki mkubwa wa wananchi katika kutoa maoni kuhusu sera mpya ya mambo ya nje.

Aidha Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Haji Janabi, aliwasihi wananchi kujitokeza kwa wingi kutoa maoni ya sera hiyo ambayo inahusu masuala ya Jamhuri ya Muungano.

Alisema Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki ni Wizara ya Muungano inayojumuisha masuala ya Zanzibar pamoja na Tanzania Bara kwa hivyo hiyo ni fursa nyingine muhimu ya kutoa maoni yao.

Kaimu Mkurugenzi wa Mambo ya Nchi za Nje katika ofisi ya Zanzibar, Balozi Silima Kombo Haji, alisema kwa upande wa Zanzibar wananchi watapata fursa ya kutoa maoni kuanzia Unguja na baadaye watendaji wa Wizara ya Mambo ya Nje watakwenda Pemba.

Alisema hivi sasa yapo mabadiliko mengi nchini pamoja na sera za kitaifa ikiwamo uchumi wa buluu pamoja na maendeleo ya lugha ya Kiswahili kuingia kimataifa zaidi yanahitajika kuingizwa katika sera hiyo mpya.

"Huu ni mchakato muhimu ambao unahusisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wananchi wetu kupata sera mpya ambayo itajumuisha mambo yote ya msingi," alisema balozi huyo. Kongamano hilo la sera mpya ya Mambo ya Nje litaongozwa na Waziri wa wizara hiyo, Januari Makamba na upande wa Kisiwa cha Pemba litaratibiwa na Naibu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk.



Mkurugenzi wa Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi, Adila Hilal Vuai, akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu kongamano la kukusanya maoni ya wadau mahususi na mapendekezo ya maboresho ya sera mpya ya mambo ya nje ya mwaka 2001, linalotarajiwa kufanyika leo katika ofisi za wizara hiyo, Maisara Zanzibar. **PICHA: ZANZIBAR**

# 'Ubunifu utumike kuondoa changamoto kwa jamii'

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said, amekitaka kituo mama cha ubunifu (IBUA Innovation Hub) kutumika kwa ubunifu ili kuondoa changamoto kwa jamii na kuleta tija kwao na taifa kwa ujumla.

Injinia Zena aliyasema hayo jana visiwani humo wakati akizindua kituo hicho na kusema ikiwa kitaondosha changamoto zinazoikabili jamii itakuwa chachu ya kuchangia upatikanaji wa maendeleo nchini.

Alikiagiza kituo hicho kutumia ubunifu kushughulikia changamoto sugu zinazoitesa jamii kama vile kuibiwa kwa rasilimali na kuikosesha serikali mapato ili kuiletea nchi maendeleo.

Alisema Zanzibar inahitaji mabadiliko makubwa kutokana na ukosefu wa ajira kwa vijana hivyo serikali inahitaji ushiriki wa sekta binafsi kuchangia ukuaji wa uchumi kupitia nyanja mbalimbali.

"Serikali inahamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika kuchangia ukuaji wa uchumi na kituo hiki kinachukua jukumu muhimu katika kukuza ushirikiano huo hivyo naamini kuwapo kwa kituo hiki itachangia uanzishaji wa vituo binafsi na kupunguza changamoto za fursa za mitaji, mafunzo, huduma za sheria na usimamizi," alisema.

Mhandisi Zena alisema kuwapo kwa kituo hicho pia ni chachu ya kuwaunganisha watafiti kutoka katika taasisi za tafiti na maendeleo kwa kufanya kazi katika miradi inayolenga kuleta ubunifu na kukuza teknolojia mpya na kuchangia ukuaji na uendelezaji wa teknolojia.

"Hii inasaidia kukuza uchumi wa kidigitali na kuwepo kwa fursa za ajira katika sekta inayokua haraka ya teknolojia na kusaidia kutatua matatizo ya kijamii kwa kuimarisha miradi inayolenga kuimarisha huduma za afya, elimu na miundombinu," alisema.

Alisema pia kuwapo kwa kituo hicho ni chachu ya kuimarisha wataalamu wa teknolojia nchini sambamba na kuchochea upatikanaji wa mbinu mpya ambazo zitachochea upatikanaji wa maendeleo.

Aliielekeza Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kuanzisha kituo kama hicho kisiwani Pemba ili kurahisishia wananchi wa kisiwa hicho kupata huduma hiyo kwa urahisi.

Naye Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango Zanzibar, Dk. Rahma Mahfoudh, alisema uwepo wa kituo hicho utasaidia kuwaunganisha wanasayansi, wahandisi, wataalamu wa teknolojia sambamba na kukuza na kuzalisha wabunifu wapya nchini.

Mkurugenzi Mkuu Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, (COSTECH) Dk. Amos Nungu, alisema taasisi hiyo ina jukumu kuendeleza ubunifu kwa kutumia njia mbalimbali ikiwamo uwepo wa kituo hicho ili kuleta tija kwa jamii na taifa.

Alisema lengo la kituo hicho ni kujenga uwezo wabunifu na wavumbuzi ili kujiendeleza na kufika malengo ya dunia katika kuelekea kwa sayansi na teknolojia.

Kituo hicho kilichoanzishwa kwa mashirikiano baina ya Tume ya Mipango na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kimegharimu shilingi milioni 135.

# Chuo kuwafuata wananchi kuwapa elimu ya sheria

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

CHUO Kikuu Mzumbe (MU), Morogoro kupitia Kitivo cha Sheria chini ya kituo cha msaada wa kisheria kinakusudia kuwafuata wananchi walipo ili kuwapatia elimu ya sheria ili kuepusha migogoro sugu ikiwamo ya ardhi, mashamba, mirathi na matunzo ya watoto.

Kaimu Mkuu wa Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu hicho, Dk. Seraphina Bakta, alisema hayo wakati akitoa elimu kwa jamii kwenye banda la kitivo hicho eneo la stendi za zamani ya daladala mjini Morogoro katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria.

Dk. Bakta alisema chuo kupitia kitivo hicho kwa sasa kimekusudia kuepusha migogoro ya wananchi kwa kushirikiana na watu mbalimbali kutoa elimu ya msaada wa kisheria katika wilaya ya Mvomero, Morogoro na Wilaya ya Njombe mkoani Njombe.

Dk. Bakta amesema kutokana na hali hiyo kitivo cha sheria tangu mwaka 2018 kimesajili kituo cha msaada wa kisheria na hilo limetokana na walimu wao wengi kuwa mawakili na wanahusika kutoa msaada wa kisheria kwa wananchi.

"Kupitia kitivo chetu msaada wa kisheria unatolewa kila wiki mara moja siku ya Ijumaa, watu waliopo kwenye maadhimisho haya endapo matatizo yao yatatatuliwa ni jambo jema na iwapo bado wanayo nafasi ya kufika kwenye kituo chetu cha msaada chuoni Mzumbe kwani kipo na ni endelevu," alisema Dk. Bakta.

Pia mwitikio wa wananchi kuvitumia kituo cha msaada wa kisheria kikiwamo cha Mzumbe bado ni mdogo kutokana na watu kupenda kuwaona wanasheria wanapokuwa wameshakwama katika matatizo yao.

"Unaweza kukuta mwananchi ameshatafuta njia mbalimbali kwenda kwa mkuu wa wilaya, mtendaji wa kata huko kote ameona hajasaidiwa ipasavyo ndipo anakuja kwenye msaada wa kisheria," alisema Dk. Bakta.

Kaimu Mkuu wa Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu hicho, amesema msaada wa kisheria unatolewa kwa mujibu wa sheria na unatolewa bure bila malipo na kwamba wananchi wanayo nafasi ya kuitumia fursa hiyo.

Dk. Bakta, alisema kituo kina shughulika pia na kutoa uwakilishi mahakamani, lakini kipaumbele kikubwa ni kutoa elimu ya sheria kwa vile kuzuia ni bora zaidi kuliko kutibu.

Dk. Bakta alisema tangu kuanzishwa kwa kituo cha msaada wa kisheria kimekuwa kikipokea kesi nyingi za wananchi zinazohusiana matatizo ya mirathi, matunzo ya watoto, ardhi, migogoro ya mashamba na nyinginezo.

"Hivi sasa kesi zinazoongoza ni za masuala ya ardhi na mambo ya mirathi," alisema.

Mmoja wa wananchi waliofika katika banda hilo kwa ajili ya kupata msaada wa kisheria, Rashida Selemani, alisema anakabiliwa na mgogoro wa kuporwa ardhi na suala hilo licha ya kulifikisha kwenye ofisi za kata, halijapatiwa ufumbuzi na kuamua kufika katika banda hilo kwa ajili ya kupata msaada wa kisheria.

Mwanafunzi wa sheria mwaka wa tatu katika chuo kikuu hicho, Denis Mnyombe, aliwashauri wananchi wenye changamoto za kisheria kutumia fursa ya kuwapo kwa timu wanasheria wa chuo kikuu hicho kwenye maonesho ya wiki wa sheria na siku ya sheria kupatiwa elimu ya sheria na ushauri wa masuala ya kesi mbalimbali.

"Jamii inakutana na kesi nyingi za jinai na za madai kama vile mirathi, talaka na ndoa, zipo kesi za mikataba ikiwamo ya ajira ni wakati mwafaka kwao kufika kwenye banda la Chuo Kikuu Mzumbe kupata elimu ya sheria na ushauri wa kisheria," alisema Mnyombe.




Ofisa Uchunguzi Kiongozi Msaidizi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB), Mkoa wa Dodoma, Faustine Malecha, akitoa elimu kuhusu kazi zinazofanywa na taasisi hiyo kwenye mkutano mkuu wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHILISO) uliofanyika jijini Dodoma mwishoni wa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mwl. mstaafu aendelea kusotea malipo yake

**Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA**

MWALIMU mstaafu Aran Jumbe, aliyewekewa kifaa maalum cha kurekebisha mapigo ya moyo, hajalipwa madai yake Sh. milioni 24.2 anayoidai Halmashauri ya Manispaa ya Singida licha ya Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, kutoa siku tano alipwe.

Januari 25, 2024 Makonda akiwa katika ziara mkoani Singida alitoa agizo kwa Manispaa ya Singida kuwa ifikapo Januari 30, 2024 fedha anazodai mwalimu huyo Sh. milioni 29.2 zilipwe kwa kuingizwa katika akaunti yake, lakini zilipofika siku tano aliingiziwa Shilingi milioni tano pekee na kubaki Sh. milioni 24.2.

Akizungumza na gazeti hili jana, mwalimu Jumbe alisema manispaa hiyo imemlipa kiasi hicho kilicho ingizwa katika akaunti yake Januari 30, mwaka huu.

Alisema baada ya kufuatilia kwa viongozi wa serikali ya wilaya na mkoa kuulizia sababu ya kulipwa kiasi hicho, Februari Mosi, Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu na Mkurugenzi wa manispaa hiyo walimwita na kumweleza kuwa watamlipa fedha nyingine mwishoni mwa mwezi Februari ili malipo yafikie asilimia 50.

Viongozi hao wa manispaa wamekiri kumwita na kumwahidi kumlipa nusu ya madai yake ifikapo mwishoni mwa mwezi Februari.

Katika mkutano wa hadhara uliofanyika stendi ya zamani mjini Singida Januari 25, mwaka huu, Jumbe ambaye ameitumikia serikali miaka 41 alimweleza Makonda kuwa toka mwaka 2019 anaidai manispaa fedha hizo bila mafanikio.

Jumbe ambaye aliugua akiwa kazini, alisema fedha hizo Sh. milioni 29.2 angelipwa kwa wakati angeweza kurudi kliniki kwa kuwa kifaa alichowekewa MOI Muhimbili kinachojulikana kama CRTD kinakaa miaka mitano na kinatakiwa kibadilishwe na gharama yake ni zaidi ya Shilingi milioni nane.

"Miaka mitano mtu anadai na amewekewa 'peacemaker' mnataka mpeleke rambirambi," alisema Makonda na kumwita Mkurugenzi Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe, kutoa maelezo na kumpa siku tano awe amemlipa fedha hizo.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida Lupembe akijibu suala hilo, alikiri mwalimu huyo kudai fedha hizo na madai yake yameingizwa serikali kuu na fedha zitakapotoka atalipwa.

Hata hivyo, Makonda alipinga sababu zilizotolewa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida na kumpa siku tano ziwe zimeingizwa kwenye akaunti yake.

# Mradi majisafi kunufaisha zaidi ya wananchi 8,000

**Na Said Hamdani, LINDI**

WANANCHI 8,949 Kata za Nangaru na Kitomanga, Wilaya ya Lindi, wanatarajia kupata majisafi na salama baada ya serikali kuridhia kutoa Sh. bilioni 2.370 kujenga miradi miwili katika vijiji vya kata hizo.

Kaimu Meneja wa RUWASA, Mhandisi Nassoro Mohamed, alisema hayo wakati wa kutia saini mikataba ya ujenzi wa miradi hiyo na Mkandarasi SCORPION wa jijini Dar es Salaam mbele ya wananchi wa vijiji husika, ukishuhudiwa na Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga.

Mohamed alisema ujenzi wa miradi hiyo itahusisha bomba kuu la kupandisha na kushusha maji nyumba ya mtambo, uwekaji wa mfumo wa umeme, tangi kuu la kuhifadhi maji, ujenzi wa Vilula kwa kila mradi maeneo ya vijiji vinavyopitiwa na mradi huo.

Alivitaja vijiji vitakavyonufaika na miradi hiyo kwa awamu ya kwanza ni Nanjime, Mkwajuni na vitongoji vyake, utatekelezwa na mkandarasi huyo kwa gharama ya Sh. bilioni 1.5, Kata ya Nangaru na maeneo ya jirani.

Alisema utekelezaji wa kazi hizo, unatarajia kuchukua muda wa miezi sita hadi kukamilika, utafanywa na mkandarasi huyo kwa gharama ya Sh. bilioni 1.3 utanufaisha wananchi 5,904.

"Hii miradi itakapokamilika itanufaisha wakazi 8,904 kutumia maji yanayotuama kwenye madimbwi ambayo sio salama," alisema Mohamedi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, aliagiza kuzingatia maagizo ya serikali kupeleka huduma ya maji katika taasisi za serikali zikiwamo shule na vituo vya kutoa huduma za afya zinafikishiwa maji.

Ndemanga alimtaka mkandarasi huyo kukamilisha miradi hiyo ndani ya muda uliopangwa kama mikataba aliyosaini inavyoelekeza.

"Mradi huu umekubali mwenyewe ndani ya miezi sita ukiwa kwenye ubora," alisisitiza Ndemanga.

Alimwagiza meneja wa RUWASA kumsimamia mkandarasi huyo kwa karibu kuhakikisha mradi unaotekelezwa unakuwa kwenye ubora unaostaili kwa wananchi wa maeneo husika.

Abdallah Hussein, Mwanahawa Ismail wakazi wa Nangaru, Zainabu Makumboila, Yunge Mwika na Alli Omari wa Mkwajuni wameishukuru serikali kuwapelekea mradi huo kwa kuwa utawaondoa katika matumizi ya maji yasiyo salama.

HABARIKIMATAIFA



Aliyekuwa Rais wa Namibia, Hage Geingob. **PICHA: MTANDAO**

# Viongozi mbalimbali wamlilia Rais wa Namibia Geingob

**Na Maulid Mmbaga**

VIONGOZI wakuu wa mataifa mbalimbali wametuma salamu za rambirambi kwa wanafamilia na wananchi wa taifa la Namibia kwa ujumla baada ya Rais wa nchi hiyo, Hage Geingob (82), kufariki dunia.

Hage Gottfried Geingob aliingia madarakani mwaka 2015, mpaka kifo chake alikuwa ni Rais wa tatu wa Namibia na alikuwa akitumikia muhula wake wa pili uliokuwa wa mwisho.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Makamu wa Rais wa Namibia, Nangolo Mbumba, kiongozi huyo aliaga dunia majira ya saa sita usiku, katika Hospitali ya Lay Pohamba jijini Windhoek alikokuwa anapatiwa matibabu ya saratani.

Miongoni mwa viongozi waliotuma salamu kutokana na msiba huo ni Rais Samia Suluhu Hassan ambaye aliandika kwenye ukurasa wake wa X akisema amehuzunishwa sana na kifo cha Rais wa Namibia Geingob, aliyemtaja kama mwanajumuiya wa Afrika na rafiki mkubwa wa Tanzania.

Rais William Ruto wa Kenya alirejea sifa hizo kwa marehemu Rais wa Namibia na kuongeza kuwa Geingob aliamini katika Afrika iliyoungana na pia alikuza mwonekano wa bara la Afrika katika nyanja ya kimataifa.

Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa alichapisha ujumbe kwenye mtandao wa X, akisema "uongozi na uimara wa Geingob vitakumbukwa".

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, alisema "Afrika Kusini inaungana na watu wa Namibia kuomboleza kifo cha kiongozi, mzalendo na rafiki wa Afrika Kusini. Akieleza kuwa Rais Geingob alikuwa mwanajeshi mkongwe wa ukombozi wa Namibia kutoka kwa wakoloni na wabaguzi wa rangi.

Ilielezwa kuwa awali alikuwa Waziri Mkuu wa Namibia baada ya nchi hiyo kupata uhuru wake ambapo alihudumu kwenye wadhifa huo kwa muda mrefu.

Pia ilibainishwa kuwa kiongozi huyo alikuwa mwanaharakati wa kupinga ubaguzi wa rangi na kabla ya kugeuka na kuwa mwanasiasa.

Makamu wa Rais wa Namibia, Angolo Mbumba, ambaye anakaimu nafasi ya Rais, alitoa wito wa utulivu, akisema Baraza la Mawaziri litakutana mara moja kutekeleza mipango muhimu ya serikali na kwamba taarifa zaidi zitatolewa.

Hata hivyo ofisi ya Rais wa Namibia ilisema Kiongozi huyo wa Nambia, Hage Geingob, aliaga dunia huku mkewe, Monica Geingob, na watoto wao wakiwa kando yake.

Vile vile Rais Mpya wa Namibia, Nangolo Mbumba, aliapishwa kuwa rais wa nne wa nchi hiyo baada ya Rais Hage Geingob kufariki hospitalini jana.

Mbumba ambaye aliwahi kuwa makamu wa Rais chini ya Geingob alikula kiapo chake cha ofisi katika ikulu ya nchi hiyo.

# 34 wauawa na shambulizi la Marekani

**WASHINGTON, Marekani**

TAKRIBANI watu 34 wakiwamo wapiganaji wanaoungwa mkono na Iran, wameuawa katika mashambulizi ya anga ya Marekani yaliyotokea usiku wa kuamkia jana nchini Iraq na taifa jirani la Syria.

Hayo yalibainishwa jana na vyanzo vya serikali na shirika linalofuatilia vita la haki za binadamu la Syria. Huku serikali ya Iraq ikisema katika taarifa yake kwamba shambulio hilo walililoliita la uchokozi wa wazi limewaua watu 16, wakiwamo raia na kuwajeruhi wengine 25.

Aidha, serikali ya Iraq ilitangaza kuwa itamwita balozi wa Marekani mjini Baghdad kupinga mashambulizi hayo.

Awali msemaji wa serikali ya Iraq Bassem al-Awadi alisema kwamba mashambulizi ya Marekani, yamepiga maeneo katika mikoa ya Akashat na Al-Qaim, ikiwamo maeneo ambako vikosi vya usalama vya nchi hiyo vimepiga kambi.

Ilielezwa kuwa Marekani ilifanya mashambulizi siku ya Ijumaa katika hatua za kulipiza kisasi kwa mauaji ya wanajeshi wake watatu katika shambulio la Droni kwenye kambi moja iliyoko nchini Jordan karibu na mpaka wa Syria na Iraq.

Washington ilidai kwamba shambulio hilo limefanywa na kundi la Islamic Resistance nchini Iraq, muungano wa wapiganaji wanaoiunga mkono Iran na kupinga uungaji mkono wa Marekani kwa Israel huko Gaza. huku kundi hilo halijadai kuhusika na shambulio hilo na Iran pia imekana kuhusika kwa namna yoyote katika shambulio.

Ikulu ya Marekani ya White House ilisema kwamba Washington ilikuwa imeionya serikali ya Iraq kabla ya shambulizi, lakini Baghdad nayo ilikataa madai ya kwamba kumekuwapo na uratibu wowote na Washington kabla ya mashambulizi.

Nalo Shirika la Haki za Binadamu la Syria limeripoti kuwa mashambulizi hayo yamewaua wapiganaji 18 wanaoungwa mkono na Iran nchini Syria. Hali ya utulivu ilikuwa inarejea kwa uangalifu siku ya Jumamosi mashariki mwa Syria karibu na mpaka na Iraq, kwa mujibu wa shirika hilo.

Pia serikali ya Iran iliyalaani mashambulizi hayo ya anga ya Marekani nchini Iraq na Syria ikisema ni kosa la kimkakati kutoka kwa hasimu wake.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Iran, Nasser Kanani, alisema katika taarifa yake kwamba shambulio la jana usiku dhidi ya Syria na Iraq ni kosa jingine la kimkakati la serikali ya Marekani, ambalo halitakuwa na matokeo yoyote zaidi ya kuzidisha hali ya wasiwasi na ukosefu wa utulivu katika kanda.

Kanani aliyataja mashambulizi ya Marekani kuwa ni ukiukaji wa mamlaka na uadilifu wa mamlaka ya Iraq na Syria, sheria za kimataifa na ukiukaji wa wazi wa katiba ya Umoja wa Mataifa.

Rais wa Marekani, Joe Biden, aliapa mashambulizi zaidi dhidi ya vituo vinavyohusishwa na Iran katika mataifa hayo mawili ya Iraq na Syria, Jeshi la Marekani katika taarifa yake limesema kuwa limevishambulia vituo zaidi ya 85 kwenye mashambulizi ya Ijumaa.

Jeshi la Marekani pia limekuwa likifanya mashambulizi ya anga dhidi ya waasi wa Kihuthi wa Yemen wanaoungwa mkono na Iran kutokana na mashambulizi dhidi ya meli za kimataifa.

Waasi wa Kihuthi walianza kulenga meli za kibiashara katika Bahari ya Shamu mnamo Novemba, wakisema wanazilenga meli zenye uhusiano na Israel kama njia ya kusaidia Wapalestina katika Ukanda wa Gaza, ambao umeharibiwa na vita vya Israel na Hamas.

Mkuu wa sera za kigeni wa Umoja wa Ulaya, Josep Borrell, ameonya juu ya kuongezeka zaidi kwa mvutano huko Mashariki ya Kati katika mkutano usio rasmi siku ya Jumamosi kufuatia mashambulizi hayo ya kulipiza kisasi ya Marekani.

**DW**

# DSTV YAUFUNGUA MWAKA NA 'PANDA TUKUPANDISHE'

**Na Mwandishi Wetu**

FEBRUARI imekuwa ya neema kwa wateja wa DStv Tanzania kutokana na kuletewa promosheni maalum ambapo kwa kipindi cha miezi miwili watakuwa wakipandishiwa vifurushi.

Katika promosheni hiyo iliyozinduliwa Februari Mosi, mwaka huu, inawawezesha wateja wa DStv wanaokidhi vigezo (wateja ambao akaunti zao zimekatika, wanaoendelea na wapya) kupata fursa ya kulipia kifurushi kinachofuatia cha juu yake na kupandishwa kwa kupatiwa kifurushi cha juu ya kile walicholipia kwa muda maalum, ambapo itadumu kwa miezi miwili na ni kwa wateja wa vifurushi vya DStv Poa, Bomba, Shangwe na Compact.

Akitangaza promosheni hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Thamani kwa Wateja Multi-Choice Tanzania, Hilda Nakajumo, alisema DStv Tanzania inafurahi kuzindua rasmi promosheni yake maalum ya 'Panda Tukupandishe' ikiwa ni njia mojawapo ya kuwashukuru wateja wao kwa kuendelea kuwa nao na pia njia ya kuwahakikishia kuwa wamejipanga vema kuendelea kuwapatia burudani isiyo na kifani.

"Mathalan, mteja wa DStv Poa Sh. 10,000 akilipia kifurushi cha juu yake ambacho ni DStv Bomba Sh. 24,000, atapandishwa na kupewa kifurushi cha DStv Shangwe Sh. 37,000/- chenye chaneli zaidi ya 100.

"Hali kadhalika, mteja wa DStv Bomba Sh. 24,000 atakayelipia kifurushi cha DStv Shangwe, atapandishwa na kupewa kifurushi cha DStv Compact chenye chaneli zaidi ya 130.

"Kwa mteja wa kifurushi cha DStv Shangwe Sh. 37,000, akilipia kifurushi cha DStv Compact atapandishwa na kupatiwa kifurushi cha DStv Compact Plus chenye chaneli zaidi ya 140, huku mteja wa kifurushi cha Compact akilipia Compact Plus atapewa kifurushi cha juu kabisa cha DStv Premium chenye chaneli zaidi ya 150," alisema Hilda.

Aidha, aliainisha kuwa promosheni hii ni kwa wateja wa DStv waliopo Tanzania, wale ambao akaunti zao ziko hai na wale ambao akaunti zao zimekatika. Pia inawahusu wateja wapya wa DStv wanaojiunga sasa na huduma hizo na kama zilivyo promosheni nyingine, kuna vigezo na masharti ambayo yatafuatwa ili mteja aweze kunufaika na promosheni hii.

Hata hivyo, wateja wa DStv ambao wamelipia kifurushi chao kwa mwaka mzima hawahusiki na promosheni hii kwani hawa tayari wana ofa yao ambapo hupata mwezi mmoja wa kifurushi chao bila malipo ya ziada.

Naye Mkuu wa Masoko MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo, alibainisha kuwa kampuni hiyo inaendelea kuwapatia wateja wake burudani ya kina bila kusahau maudhui mengine kama habari na elimu, huku ikihakikisha kuwa wateja wake wanapata maudhui kemkem na ya kusisimua ya ndani na nje.

Shelukindo amesema kuwa kunufaika na promosheni hii ni rahisi kwani mteja anachotakiwa kufanya ni kulipia kifurushi cha juu ya kile anachotumia na DStv itamzawadia kifurushi cha juu zaidi.




Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo, akizungumza wakati wa uzinduzi rasmi wa Promosheni ya ,Panda Tukupandishe', maalum kwa ajili ya wateja wa DStv, iliyofanyika jijini Dar es Salaam wiki iliyopita. Promosheni hiyo kabambe ilianza rasmi Februari Mosi na itadumu hadi Machi 31, mwaka huu. **MPIGAPICHA WETU**

# Malindi yadundwa, yaigeukia Ngome

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Malindi SC imeanza vibaya Ligi Kuu ya Zanzibar mzunguko wa lala salama kwa kuambulia kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Wanajeshi wa Kipanga FC.

Bao pekee la Wanajeshi wa Kipanga lilifungwa na mchezaji Akram Ahmed Zubeir katika dakika ya 58 kwenye mchezo huo uliochezwa juzi katika Uwanja wa Mau A.

Akizungumza na Nipashe Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Suleiman Mohmed 'Mo', alisema kufungwa katika mchezo huo kumetokana na makosa madogo yaliyofanywa na safu ya ulinzi.

Alisema timu yake ilicheza vizuri katika dakika zote za mchezo licha ya mchezo huo kuwa mgumu kwani hata wapinzani wao walitumia mbinu ya kulinda zaidi lango lao ili kuzuia mashambulizi yanayoelekezwa kwao mbinu ambayo kwao ilifanikiwa.

Alisema kupoteza katika mchezo huo muhimu haina maana kama wamevunjika moyo, bali imewapa hari na hamu ya kuhakikisha mchezo unaofuata wanapata alama tatu ili kuzichanga alama ambazo zitawafanya kutoka katika mstari mwekundu wa kushuka daraja.

"Katika soka makosa madogo unayoyafanya basi yanaweza kuigharimu timu hasa katika matokeo, wachezaji walijitahidi kujituma na kucheza vizuri na kwa mipango, lakini bahati ilikuwa kwa upande wa wapinzani wetu," alisema.

Aidha, alisema kuwa hivi sasa wanaelekeza mipango yao katika mchezo wao wa 17 dhidi ya Ngome utakaopigwa Alhamisi wiki hii.

"Tunaenda kukutana na timu ambayo inaburuza mkia katika Ligi Kuu Zanzibar, mchezo huu utakuwa mgumu sana kama vile unacheza na timu ambayo ipo katika mbio za ubingwa, hivyo lazima tujipange na umakini uongezeke kwa wachezaji ili kupata matokeo mazuri," alisema.

Alisema ili kufanikiwa lengo la kupata alama tatu wataenda kurekebisha makosa kadhaa ambayo wameyaona kupitia mchezo wao dhidi ya Kipanga hasa suala la umakini mchezoni.

Naye Kocha wa Kipanga FC, Hassan Abdulrahman, alisema licha ya kutoka na ushindi mwembamba, mchezo huo ulikuwa mgumu.

"Unapocheza na timu ambayo ipo katika hatari ya kushuka daraja, mchezo unakuwa mgumu sana kwa sababu yeye anataka alama za kumtoa alipo na kumpandisha juu, hivyo lazima kama mwalimu tulisoma mbinu za wapinzani wetu mapema na kufanikiwa," alisema.

Katika mchezo mwingine wa ligi hiyo uliopigwa Uwanja wa Mau B, Mabaharia wa KMKM SC walipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Maafande wa Uhamiaji wakati katika Uwanja wa Finya, Hard Rock walitumia vizuri dhidi ya Ngome FC baada ya kuibuka ya kushinda 1-0.

# St Mary's wajenga viwanja vya kisasa kuibua vipaji

**Na Joseph Mwendapole**

KATIKA jitihada za kuinua sekta ya michezo nchini, Shule ya Sekondari St Mary's, imejenga viwanja vya kisasa vya michezo ikiwamo kiwanja cha mpira wa miguu shuleni hapo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa shule hiyo, Reca Ntipoo, wakati wa hafla ya kuwapongeza wanafunzi wa shule hiyo waliopata daraja la kwanza kwenye mitihani ya kitaifa ya kidato cha nne.

Alisema shule hiyo imebaini kuwa michezo ni muhimu kwa ajili ya kuibua vipaji mbalimbali vya wanafunzi ndiyo maana ikaamua kujenga viwanja vya michezo vya kisasa ili kuibua vipaji.

"Tuna viwanja vya mpira vya kisasa, mpira wa mikono, wavu na tutaendelea kuimarisha michezo shuleni kwa sababu mwanafunzi anaposhiriki michezo hata akili yake inachangamka," alisema na kuongeza.

"Kwenye matokeo ya kidato cha nne tumepata daraja la kwanza, daraja la pili na wachache daraja la tatu na tumeona namna michezo ambavyo inachangia kuwachangamsha wanafunzi kuwa weledi darasani," alisema Ntipoo.

Reca alisema shule hiyo imepanga muda maalum kwa wanafunzi kushiriki michezo mbalimbali kama mpira wa miguu mpira wa mikono sarakasi na skauti.

"Shule pamoja na kufanya vizuri kitaaluma imeona umuhimu wa kujenga viwanja vya Volley Ball, mpira wa miguu na mpira wa kikapu, sisi masuala ya michezo hatuyachukulii poa kwa sababu tunafahamu kwamba michezo ni uchumi kwani wapo watu ambao wanaingiza mabilioni kupitia vipaji kwenye michezo mbalimbali," alisema.

"Na tunaushukuru sana viongozi wa shule kwa kutuunga mkono kwenye michezo na kwenye viwanja hivi wameweka taa kubwa kama zinazotumika kwenye viwanja vikubwa vya michezo hali ambayo inasaidia wanafunzi kufanya mazoezi hata nyakati za usiku," alisema

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### FERNANDE AIKATAA AL-HILAL
KIUNGO wa kati wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ureno, Bruno Fernandes, mwenye umri wa miaka 29, amekataa ofa kutoka Klabu ya Saudi Arabia Al-Hilal katika dirisha la uhamisho la Januari. **(Record via Manchester Evening News)**

### SANE KUBAKI BARCA
WINGA wa Ujerumani, Leroy Sane, mwenye umri wa miaka wa 28, anatarajiwa kukataa ombi la Liverpool, Chelsea na Barcelona badala yake anatarajia kukubali mkataba mpya Bayern Munich. **(Sport)**

### HALL ATAKIWA MAN CITY
KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, ametuma maofisa kwenda kumtathmini kiungo wa kati wa Tottenham Horspur, Tyrese Hall. **(Football Transfers)**

### LOKONGA SASA KUUZWA
ARSENAL imeamua kumuuza kiungo wa kati wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 24, Albert Sambi Lokonga, katika msimu unaowadia wa majira ya joto, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo Luton. **(Football Insider)**

### CHOLABAH KUBAKI CHELSEA
ALIYEKUWA mchezaji wa Timu ya Taifa ya England, Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 24, yuko tayari kubaki Chelsea na kutetea nafasi yake katika kikosi cha Mauricio Pochettino. **(Caught Offside)**

### TOMIYASU MKATABA MPYA
KLABU ya Arsenal inajitayarisha kusaini mkataba mpya na mlinzi wa Japan, Takehiro Tomiyasu wakati mchezaji huyo wa miaka 25 atakaporudi kutoka mashindano ya Kombe la Asia. **(Fabrizio Romano)**

### GILL KAAMUA KUBAKI
WINGA wa Hispania, Bryan Gil alikuwa akihusishwa na uhamisho wa mkopo Januari, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ameamua kubaki Tottenham Hotspur. **(Fabrizio Romano)**

### SENSI, LEICESTER BADO
UHAMISHO wa mkopo wa kiungo wa kati wa Italia, Stefano Sensi kutoka Inter Milan kwenda Leicester City umezimwa licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, kufaulu vipimo vya afya Alhamisi. **(Telegraph)**

### SELS AJIUNGA FOREST
KLABU ya Nottingham Forest imemsajili mlinda mlango wa Ubelgiji, Matz Sels kutoka Strasbourg ya Ufaransa ya Ligue 1 kwa ada ya takriban pauni milioni tano. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amejiunga kwa mkataba wa miaka mitatu na nusu. **(BBC Sport)**

### UNAL ATUA BOURNEMOUTH
KLABU ya Bournemouth imemsajili mshambuliaji wa Uturuki, Enes Unal, kwa mkopo kutoka Getafe. Unal mwenye umri wa miaka 26, amefunga mabao 36 kwenye mechi 109 katika klabu hiyo ya LaLiga tangu ajiunge nayo kutoka Villareal mwaka 2020. **(BBC Sport)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MBAPPE AAMUA ATAJIUNGA REAL

Mshahara wake huko Madrid, unatarajiwa kuwa nusu ya kile anachopata sasa PSG...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe ameamua kujiunga na Real Madrid mara tu mkataba wake na Paris Saint-Germain utakapomalizika msimu huu wa majira ya joto, vyanzo vimethibitishwa kwa ESPN.

Habari hiyo iliripotiwa kwa mara ya kwanza na gazeti la Le Parisien.

Mwezi uliopita, ESPN iliripoti kwamba Mbappe amepewa mkataba na Madrid na, kulingana na chanzo, anatarajiwa kutangaza uamuzi wake wa kujiunga na mabingwa hao mara 14 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki ijayo.

Mbappe mwenye umri wa miaka 25, bado hajaifahamisha PSG wala Real Madrid, vyanzo vilisema, lakini huo ndio uamuzi wake.

Nia yake ya kuruhusiwa kucheza na Ufaransa katika Michezo ya Olimpiki kwenye ardhi ya nyumbani majira ya joto, itakuwa sehemu muhimu ya mazungumzo na Madrid.

Na kwa kuzingatia mabadiliko ya awali ya Mbappe juu ya kuhamia Bernabeu mnamo 2022, kuna uwezekano kila wakati kwamba anaweza kubadilisha mawazo yake hadi makubaliano yatiliwe saini na pande zote mbili.

Hata hivyo, uhamisho wake wa kwenda Madrid sasa unaelekea kutimia msimu huu wa majira ya joto.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba PSG ilimpa Mbappe nyongeza ya mshahara wa jumla wa euro milioni 72, lakini pendekezo lao lilikataliwa na mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa.

Vyanzo vilivyoshauriwa na ESPN vilisema kwamba kwa kuchagua kuondoka kwenye klabu kama mchezaji huru, Mbappe atachagua kutopokea bonasi ambazo ni karibu euro milioni 100.

Mshahara wake huko Madrid, kulingana na chanzo, unatarajiwa kuwa nusu ya kile anachopata sasa PSG.

Nahodha huyo wa Ufaransa, ambaye alikua anavutiwa sana na nguli wa Bernabeu, Zinedine Zidane na Cristiano Ronaldo, amekuwa na ndoto ya kuichezea Madrid na, kulingana na chanzo, anahisi ni wakati muafaka katika maisha yake ya soka kuhamia mji mkuu wa Hispania.

Kwa kuwa sasa mustakabali wake umeamuliwa, PSG itafuata mpango wao B na kulingana na vyanzo, wamemtambua Rafael Leao wa AC Milan kama mbadala wa Mbappe.

# WILLIAMS AKUNWA KWA KIWANGO AFRIKA KUSINI



**ABIDJAN, Ivory Coast**

GOLIKIPA namba moja wa Afrika Kusini, Ronwen William, aliwasifia wachezaji wenzake wote na benchi la ufundi kwa kiwango bora Jumamosi bada ya kufuzu nusu fainali kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika, Afcon.

Kipa huyo sio tu kwamba aliizuia Cape Verde katika dakika 120 za mchezo, lakini zaidi aliokoa penalti nne za 'Blue Sharks' hao.

Mchezo huo ulilazimika kuamuliwa kwa mikwaju ya penalti baada ya dakika 90 na zile 30 za nyongeza kumalizika bila bao.

Na Afrika Kusini wakapata penalti mbili dhidi ya moja ya Cape Verde na kutinga nusu fainali na sasa watakutana na Nigeria.

"Ilikuwa ngumu. Walicheza sehemu yao na ulikuwa wakati wangu wa kucheza sehemu yangu," alisema William akiwapongeza wachezaji wenzake na benchi la ufundi.

"Nina furaha kwamba tuko katika raundi inayofuata. Hii sio yangu lakini ni ya pamoja.

"Wchezaji na timu ya ufundi. Safari hii imekuwa ngumu, lakini tulishiriki kama timu kwa hiyo nitakubali hili kwa niaba ya kila mchezaji wa Bafana Bafana," alisema Williams.

Bafana Bafana watamenyana na Super Eagles katika nusu-fainali Jumatano katika Uwanja wa Paix mjini Bouake.

# Diakite sasa awashukuru mashabiki wa Ivory Coast

**ABIDJAN, Ivory Coast**

KIUNGO wa Ivory Coast, Oumar Diakite amewashukuru mashabiki wa nyumbani kutokana na ushindi wao dhidi ya Mali katika robo fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), juzi Jumamosi.

Diakite ambaye alifunga bao la ushindi alikiri mchezo huo ulikuwa mgumu, lakini walikuwa na mashabiki wao wa nyumbani ambao waliwaunga mkono kwa muda wote wa dakika 120.

"Mashabiki walifanya walichopaswa kufanya na tangu mashindano haya yaanze, tumeona uungwaji mkono wa Ivory Coast, wamekuwa na sisi muda wote.

"Leo (juzi) tulikuwa na wakati mgumu kwenye mchezo ikiwa ni pamoja na kadi nyekundu, lakini waliendelea kutusukuma na kwa sisi kama wachezaji, wakati mambo yanapoanza kuwa hivyo, tuna chaguo la kujitolea zaidi," alisema.

Ivory Coast walimpoteza mchezaji mmoja kwa kadi nyekundu katika kipindi cha kwanza. Hata hivyo, walifanikiwa kurejea mchezoni na kushinda katika hatua za mwisho za muda wa ziada.

Diakite aliongeza kuwa walijua mchezo utakuwa mgumu baada ya kadi nyekundu.

"Tulijua itakuwa ngumu, ilifanya iwe ngumu kwetu, lakini tuliweza kufanya kile tunachotaka na mawazo yetu.

"Tulikimbia na tulifanya juhudi na nadhani tulilipwa mwisho wa siku na sote tulijitoa kupata ushindi huu maalum, tunafurahi, kwa sababu nilifunga bao la pili.

"Kwa bao lile nadhani niliweka furaha kwenye nyuso za mashabiki wa Ivory Coast wapatao 30,000 waliokuwa uwanjani. Hakuna maneno yanayoweza kuelezea jinsi ninavyohisi hivi sasa, lakini nina furaha," aliongeza.



# Xavi alia waamuzi wa LaLiga kuionea Barcelona

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez, amewasihi waamuzi wa LaLiga "watuache tushindane" na kudai klabu hiyo ya Katalunya "inalipia kesi ya Negreira" baada ya kadi nyekundu ya Vitor Roque katika ushindi wa 3-1 Jumamosi dhidi ya Alaves.

Roque alitolewa nje kwa kadi nyekundu dakika 13 tu baada ya kuingia uwanjani baada ya kupewa kadi mbili za njano pia akifunga bao la tatu.

Xavi alilalamika kuwa ni moja ya maamuzi mengi yanayoiumiza Barca msimu huu na akasema timu yake inaona matokeo ya uchunguzi wa uhusiano wao na makamu wa rais wa zamani wa bodi ya waamuzi ya Hispania, Jose Maria Enriquez Negreira ndio sababu.

Barca ililipa kampuni inayohusishwa na Negreira zaidi ya euro milioni 7 katika kipindi cha miaka 18, lakini wanashikilia kuwa walikuwa wakinunua ripoti za kiufundi kutoka kwa waamuzi na hawakuwahi kuwahonga maofisa wa mechi au kutoa ushawishi wowote.

"Ni makosa ya mwamuzi dhidi yetu – haikuwa haki, ikiwa tunasema ukweli," alisema Xavi, ambaye na aliongeza kuwa Barca itakata rufani dhidi ya kadi nyekundu.

"Ninaomba tu waamuzi waturuhusu tushiriki LaLiga. Hiki ni kisa kingine cha makosa ya wazi dhidi ya Barca. Kila mtu anaweza kuona ukweli.

"Tunalipia kesi ya Negreira, hakuna shaka. Lakini ndivyo hivyo, sitazungumza kuhusu waamuzi tena."

Maoni ya Xavi yamekuja saa 24 tu baada ya kuishutumu Real Madrid TV kwa "kushawishi mashindano kila wiki" kwa kutangaza video zinazoangazia makosa ya waamuzi kabla na baada ya mechi msimu huu.

Hilo lilimfanya kocha wa Madrid, Carlo Ancelotti kusema kwamba hutazama kwenye kiwango cha Barca baada ya rais wa Blaugrana hao, Joan Laporta pia kusema Real Madrid "hawako vizuri" katika mahojiano ya Ijumaa.

"Nina uhusiano mzuri na Ancelotti," Xavi alijibu. "Hii haihusiani naye. Nina heshima kamili kwa Ancelotti."

HABARI MICHEZO

# JKT QUEENS YAPOKWA POINTI TANO, SIMBA QUEENS KILELENI

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya JKT Queens imenyang'anywa pointi tano na kupigwa faini ya Sh. milioni tatu, baada ya kudhihirika kuwa iligomea mchezo dhidi ya Simba Queens uliokuwa uchezwe Januari 9, mwaka huu, katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), na kusainiwa na Ofisa Habari na Mawasiliano, Cliford Ndimbo, imeeleza kuwa adhabu hiyo imetolewa na Kamati ya Soka la Wanawake katika kikao chake ilichokaa na kupitia taarifa mbalimbali za michezo ya Ligi Kuu ya Wanawake na kutoa maamuzi.

Kamati hiyo pia imeipatia Simba Queens pointi tatu na mabao matatu kwa mujibu wa Kanuni ya 18:45 ya Ligi ya Wanawake toleo la 2023.

Taarifa hiyo imesema baada ya kupitia taarifa hizo, kamati imeipoka JKT Queens pointi tano na kuipiga faini hiyo kutokana na kujiridhihisha pasipo shaka kuwa klabu hiyo ilipata taarifa ya mchezo huo husika kuchezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kabla ya siku ya mchezo, Januari 8 katika kikao cha maandalizi ya mchezo.

Aidha, kamati hiyo imemfungia mwaka mmoja, Katibu Mkuu wa JKT Queens, Duncun Maliyabwana, kujuhusisha na shughuli za mpira wa miguu kwa kipindi hicho.

Siku ya tukio, timu hizo zilipaswa kucheza mechi Uwanja wa Azam Complex, Chamazi ambako waamuzi walikwenda, lakini timu ya JKT Queens haikutokea, badala yake ilikwenda Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo ikidai kuwa ndiyo uwanja wao wa nyumbani, pia viongozi wa klabu hiyo wakidai hawakupata taarifa yoyote ya kuhamishwa uwanja.

Kutokana na uamuzi huo, Simba Queens iliyokuwa na pointi 19 na mabao 27 na kushika nafasi ya pili, sasa inakuwa imejikusanyia pointi 22 na mabao 30, ikienda juu ya msimamo wa ligi hiyo.

Baada ya kunyang'anywa pointi hizo, JKT Queens iliyokuwa na pointi 21 ikiongoza ligi, sasa imebakiwa na pointi 16, ikishuka hadi nafasi ya pili ya msimamo.

SHUJAA...



Kipa na nahodha wa Timu ya Taifa ya Afrika Kusini, Ronwen Williams, akicheza moja kati ya penalti nne alizookoa wakati wakishinda kwa mikwaju ya penalti 2-1 dhidi ya Cape Verde juzi kwenye mechi ya robo fainali ya michuano ya Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023, zinazoendelea nchini Ivory Coast. **PICHA: MTANDAO**

# FA Cup Zanzibar kutimua vumbi leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MICHUANO ya Kombe la ZFF (FA CUP), kwa upande wa kisiwani Pemba yanaanza kutimua vumbi leo Jumatatu.

Michuano hiyo kwa kisiwani humo inashirikisha timu 20 kwa hatua ya awali ambayo itazikutanisha timu kutoka mikoa miwili ya Pemba ambayo ni Kaskazini na Kusini pamoja na timu kutoka Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba huku ikichezwa katika viwanja viwili vya Ngerengere na Finya.

Kwa mujibu wa ratiba ya michuano hiyo katika kila uwanja kutakuwa na mechi mbili ambazo zitachezwa saa 8:00 mchana na saa 10:00 alasiri, isipokuwa Februari 7 na 8 kutakuwa na michezo itakayochezwa saa 10 pekee katika viwanja vyote viwili vinavyotumika kuchezea michuano hiyo.

Katika Uwanja wa Ngerengere wakati wa saa 8:00 mchana Mila FC itacheza na Mkoroshoni na saa 10:00 alasiri Mbuzini itachuana na Yosso Boys, wakati katika Uwanja wa Finya saa 8:00 mchana New Star itakwaruzana na Mwenge na saa 10:00 alasiri Imara itakutana uso kwa uso na El-gado.

Siku inayofuata kutakuwa na michezo minne ambapo katika Uwanja wa Ngerengere saa 8:00 Mgogoni itapambana na Al-azar na saa 10:00 Tibirinzi itakwaana na FFC.

Katika Uwanja wa Finya siku hiyo majira ya saa 8:00 Kifumbikai FC watacheza na New Stone na saa 10:00 Dynamoo itacheza na Jifunze. Timu nyingine ambazo zinashiriki michuano hiyo ni Tekeleza, Wawi Star, Kizimbani, Chakechake, Machomanne, Danger Boys, Junguni na Azimio, zitakazocheza Februari 8, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Kanuni ya Mashindano hayo, michuano hiyo inasimamiwa na Kamati ya Mashindano ambapo Mshindi wa Kanda ya Pemba atakutana na Mshindi wa Kanda ya Unguja kupata timu itakayoiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

## Simba yafichua sababu ushindi

INATOKA UK. 24

"Kitu kingine kilichosababisha mechi iwe ngumu ni kwa sababu Mashujaa FC wapo chini na wanataka kujinasua kushuka daraja na ukiangalia hiki kilichocheza si kikosi ambacho walianza nacho kwenye ligi, zaidi ya wachezaji 18 wameingizwa, tena ni wachezaji ambao ni wazoefu na wanaijua ligi ya Tanzania, tulijua mechi itakuwa ngumu kutokana na aina ya wachezaji ambao imewachukua," alisema.

Baadhi ya wachezaji wapya kwenye kikosi hicho na waliocheza kwenye kikosi cha kwanza ni Abdulrahman Mussa, Reliants Lusajo, Mpoki Mwakinyuke na wengineo.

Kocha wa Mashujaa FC, Mohamed Abdallah ‚Bares', aliwapongeza Simba kwa ushindi, lakini akiwasifu vijana wake kwa kucheza vile ambavyo aliwaagiza.

„Vijana wamecheza vizuri na wametekeleza kile ambacho tuliwatuma, tumepoteza kwa sababu ya kosa la kimpira, penalti ndiyo iliyotuhukumu.

Tumekuja kupambana na Simba, tumefanya kadri ya uwezo wetu, lakini tumeshindwa, tuna wachezaji wengi wapya ambao wanahitaji muunganiko, naamini huko mbele ya safari tutakuwa vizuri zaidi, hasa eneo la ushambuliaji," alisema kocha huyo.

Bao pekee la Simba lilifungwa dakika ya 15 na Saido Ntibazonkiza kwa mkwaju wa penalti likiiwezesha kufikisha pointi 26 ambazo hata hivyo hazikutosha kuwaondoa kwenye nafasi ya tatu na Mashujaa FC pia ikasalia nafasi 15 na pointi zake tisa.

## Yanga hesabu kwa Dodoma Jiji FC leo

INATOKA UK. 24

na wachezaji ambao wako katika timu hiyo, wakati huu akiendelea kumkosa kipa wake namba moja, Djigui Diarra, ambaye alikuwa na timu yake ya Mali iliyoondolewa na wenyeji, Ivory Coast katika michuano ya AFCON juzi.

Kocha wa Dodoma Jiji FC, Baraza yeye alisema amefanikiwa kuwaona Yanga katika mechi iliyopita dhidi ya Kagera Sugar, kuona ubora na madhaifu yao na tayari amemaliza kazi yake na jukumu kubwa amewaachia wachezaji wake.

Alisema ameona ubora wa Yanga ikiwamo uimara wa safu yao ya viungo washambuliaji huku wakimtumia mara kadhaa Pacome Zouzoua kushambuliaji, jambo ambalo wamelifanyia kazi pamoja na kila nafasi, wanashuka dimbani kwa ajili ya kuonyesha mchezo mzuri.

"Tuna waheshimu Yanga, ni timu nzuri ina wachezaji wazuri, lakini tumejipanga vizuri kwa ajili ya kuleta ushindani mkubwa kuhakikisha tunafanikiwa kuvuna alama muhimu mbele ya wenyeji wetu hao," alisema Baraza.

# Michezo

Jumatatu Februari 5, 2024

Nipashe


## Mbappe sasa aamua atajiunga Real Madrid

UKURASA 21



## BADO CONGO...!



Mshambuliaji wa Ivory Coast, Oumar Diakite (aliyevua shati), akishangilia sambamba na wachezaji wenzake baada ya kuifungia timu yake bao la ushindi dakika ya 120, wakati wakishinda 2-1 dhidi ya Mali, kwenye mechi ya robo fainali ya Fainali za Mataifa ya Afrika iliyopigwa nchini humo juzi. Ivory Coast ambao ni wenyeji wa michuano hiyo, nusu fainali sasa itakutana na DR Congo keshokutwa, Jumatano, siku hiyo pia Nigeria itavaana na Afrika Kusini. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA HESABU KWA DODOMA JIJI FC LEO

### Gamondi asema haitakuwa rahisi, lakini amefanyia kazi makosa ya mechi...

**Na Saada Akida**

WAKATI Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, wakishuka Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam leo saa moja usiku kuikaribisha Dodoma Jiji FC, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Miguel Gamondi, amesema „haitakuwa mechi rahisi", lakini wamejipanga kuondoka na alama tatu.

Kikosi cha Yanga kinashuka dimbani kikiwa na kumbukumbu ya kutoka suluhu mchezo uliopita ugenini katika Uwanja wa Kaitaba, Bukoba dhidi ya Kagera Sugar, ambapo leo kimedhamiria kuendeleza ubabe wao katika Dimba la Azam Complex ambapo mara ya mwisho kiliibuka na ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Hausing FC, kwenye Kombe la FA.

Hata hivyo, wakati Yanga ikipigia hesabu alama tatu za mchezo huo, Dodoma Jiji FC inayonolewa na Kocha Francis Baraza, nayo imedhamiria kutafuta alama muhimu mbele ya vigogo hao baada ya kueleza kuwa imewasoma na kuona ubora na mapungufu yao.




Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Yanga, Gamondi amesema baada ya suluhu dhidi ya Kagera Sugar, wamesahihisha makosa yao na kujiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo huo dhidi ya Dodoma Jiji FC.

Alisema mechi haitakuwa rahisi kwa kuwa kila timu imejiandaa vizuri, lakini wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya kutafuta alama muhimu ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kufikia malengo yao ya kutetea ubingwa.

"Sasa tumerejea baada ya kutoka Kagera katika mchezo mgumu, tumefanyia kazi mapungufu, ikiwamo kutumia nafasi zinazopatikana, tumejipanga vizuri kukabiliana na wapinzani wetu, Dodoma Jiji FC ni wazuri na tutacheza kwa heshima kubwa," alisema Gamondi.

Aliongeza kuwa anaendelea kufanya mabadiliko ya kikosi chake kulingana

INAENDELEA UK. 23

# Simba yafichua sababu ushindi kiduchu Kigoma

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, amesema ushindi wa bao 1-0 ilioupata juzi kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma, ulitokana na kuamua kubadilisha mfumo kuendana na aina ya uwanja ulivyo.

Matola alisema hawakucheza kwenye mfumo wao wa kawaida uliozoeleka kutokana na uwanja haukuwa rafiki kwao, hivyo kwa muda mrefu kulazimika kupiga mipira ya juu na kumsimamisha straika mmoja Freddy Michael Kouablan mbele na kuimarisha viungo katikati na hii imewasaidia kupata ushindi kwenye mechi ngumu.

„Haikuwa mechi rahisi, ilikuwa ngumu sana, niwapongeze wachezaji wetu tulihitaji pointi tatu na tumezipata haijalishi tumezipata kwa namna gani, tumetimiza yale ambayo tulihitaji kuyatimiza Kigoma, kipindi cha kwanza kama tungekuwa makini tungeweza kupata hata mabao mawili, hata hivyo uwanja haukuwa mzuri sana ndiyo maana mara nyingi tulicheza mipira ya juu, tukaweka straika mwenye nguvu pale kati, na kama uliona tuliimarisha sana safu ya viungo pale kati ili mradi tu kwenye viwanja kama hivi ambavyo si rafiki tuweze kucheza kwa kupambana na si ufundi sana," alisema Matola.

Simba ilianzisha viungo wakabaji watatu katika mechi hiyo ambao ni Babakar Sarr, Mzamiru Yassin na Sadio Kanoute kwa wakati mmoja.

Matola aliwasifu wachezaji wa Simba kwa kupambana hadi dakika ya mwisho, akisema mechi haikuwa rahisi kutokana na wapinzani wao kusajili wachezaji wengi wapya na wazoefu hasa kipindi cha usajili wa dirisha dogo.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >